JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# SERA YA TAIFA YA JINSIA NA MAENDELEO YA WANAWAKE YA MWAKA 2023

OKTOBA, 2023

# YALIYOMO


**VIFUPISHO** ........ **iii**
**TAFSIRI YA MANENO** ........ **v**
**DIBAJI** ........ **vi**
**SURA YA KWANZA** ........ **1**
**UTANGULIZI** ........ 1
1.1 Usuli ........ 1
1.2 Hali ilivyo katika Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 ........ 4
1.2.1 Utekelezaji wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ........ 4
1.2.2 Mafanikio ........ 19
1.2.3 Upungufu ........ 20
1.2.4 Changamoto ........ 20

**SURA YA PILI** ........ **22**
**UMUHIMU WA SERA, DIRA, DHIMA NA MALENGO** ........ **22**
2.1 Umuhimu wa Sera ........ 22
2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera ........ 22
2.2.1 Dira ........ 22
2.2.2 Dhima ........ 23
2.2.3 Lengo la Sera ........ 23
2.2.4 Malengo Mahsusi ........ 23

**SURA YA TATU.** ........ **24**
**MASUALA YA KISERA, MALENGO NA MATAMKO.** ........ **24**
3.1 Utangulizi ........ 24
3.2 Masuala ya Kisera ........ 24
3.2.1 Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi ........ 24
3.2.2 Ukatili wa Kijinsia ........ 25
3.2.3 Haki na Usawa Kiuchumi ........ 26
3.2.4 Jinsia, Uongozi na Maamuzi ........ 27
3.2.5 Jinsia, Elimu na Mafunzo ........ 28
3.2.6 Jinsia na Afya ........ 28
3.2.7 Jinsia, Teknolojia na Ubunifu ........ 29
3.2.8 Takwimu za Kijinsia ........ 31
3.2.9 Wanawake, Amani na Usalama ........ 31
3.2.10 Masuala Mtambuka ........ 32

**SURA YA NNE** ..... **35**
**MUUNDO WA KISHERIA** ..... **35**

**SURA YA TANO.** ..... **36**
**MUUNDO WA KITAASISI** ..... **36**
5.1 Utangulizi ..... 36
5.2 Majukumu ya Wadau ..... 36
5.2.1 Wizara yenye Dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ..... 36
5.2.2 Wizara yenye Dhamana na Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu ..... 37
5.2.3 Wizara yenye Dhamana na Fedha ..... 37
5.2.4 Wizara yenye Dhamana na Mazingira ..... 38
5.2.5 Wizara yenye Dhamana na Maji ..... 38
5.2.6 Wizara yenye Dhamana na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ..... 38
5.2.7 Wizara yenye Dhamana na Ardhi ..... 38
5.2.8 Wizara yenye Dhamana na Kilimo ..... 38
5.2.9 Wizara yenye Dhamana na Mifugo na Uvuvi ..... 39
5.2.10 WizarayenyeDhamananaMichezo ..... 39
5.2.11 Wizara yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. ..... 39
5.2.12 Wizara yenye Dhamana na Katiba na Sheria ..... 40
5.2.13 Wizara yenye Dhamana na Ulinzi na Usalama ..... 40
5.2.14 Wizara yenye Dhamana na Ujenzi ..... 40
5.2.15 Wizara yenye Dhamana na Uchukuzi ..... 40
5.2.16 Wizara yenye Dhamana na Nishati ..... 40
5.2.17 Wizara yenye Dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi ..... 41
5.2.18 Wizara yenye Dhamana na Uwekezaji na Mipango ..... 41
5.2.19 Wizara yenye Dhamana na Viwanda na Biashara ..... 41
5.2.20 Wizara yenye Dhamana na Utumishi na Utawala Bora ..... 41
5.2.21 Wizara yenye dhamana na Madini ..... 42
5.2.22 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ..... 42
5.2.23 Sekretarieti za Mikoa ..... 42
5.2.24 Mamlaka za Serikali za Mitaa ..... 42
5.2.25 Bunge ..... 43
5.2.26 Asasi za Kiraia/Bodi za Kitaalam ..... 43
5.2.27 Sekta Binafsi ..... 44
5.2.28 Taasisi za Elimu na Utafiti ..... 44
5.2.29 Wadau wa Maendeleo ..... 45
5.2.30 Vyombo vya Habari ..... 45
5.2.31 Familia na Jamii ..... 45
5.3 UfuatiliajinaTathmini ..... 45
5.4 Hitimisho ..... 47

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| ALSD | - | Alternative Learning Skills Development |
| ASCAs | - | Accumulated Savings and Credit Associations |
| AU | - | African Union |
| AU CRF | - | African Union Continental Result Framework |
| AZAKI | - | Asasi za Kiraia |
| BBT | - | Building a Better Tomorrow |
| BPfA | - | Beijing Declaration and Platform for Action |
| CEDAW | - | Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination Against Women |
| iCHF | - | Improved Community Health Fund |
| CLF | - | Converged Licensing Framework |
| COWSOs | - | Community Owned Water Supply Organizations |
| CSR | - | Cooperate Social Responsibility |
| CSW | - | Commission on the Status of Women |
| DADP | - | District Agricultural Development Program |
| DHS | - | Demographic and Household Survey |
| EAC | - | East Africa Cooperation |
| ESDP | - | Education Sector Development Plan |
| EWURA | - | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| FGM | - | Female Genital Mutilation |
| GBV | - | Gender Based Violence |
| GEWE | - | Gender Equality and Women Empowerment |
| GII | - | Gender Inequality Index |
| GRB | - | Gender Responsive Budgeting |
| GVM | - | Gross Vehicle Mass |
| HESLB | - | Higher Education Students' Loans Board |
| HIV | - | Human Immunodeficiency Virus |
| ICT | - | Information Communication Technology |
| ILFS | - | Integrated Labour Force Survey |
| IPA | - | Institutional Plan of Action |
| ISNGP | - | Implementation Strategy for National Gender Policy |
| JMT | - | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| LGAs | - | Local Government Authorities |
| LPG | - | Liquified Petroleum Gas |

| | | |
|---|---|---|
| MDGs | - | Millennium Development Goals |
| MIS | - | Management Information System |
| MKUKUTA | - | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MMT | - | Methadone Maintenance Treatment |
| MTAKUWWA | - | Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto |
| NBS | - | National Bureau of Statistics |
| NCD | - | Non-Communicable Disease |
| NECP | - | National Employment Creation Programme |
| NEEC | - | National Economic Empowerment Council |
| NFP | - | National Forest Programme |
| NHIF | - | National Health Insurance Fund |
| SACAs | - | Savings and Credit Associations |
| PMTCT | - | Prevention from Mother to Child Transmission |
| SACCOs | - | Savings and Credit Cooperative Society |
| SADC | - | Southern African Development Community |
| SDGs | - | Sustainable Development Goals |
| SIGI | - | Social Institutions and Gender Index |
| STEM | - | Science, Technology, Engineering and Mathematics |
| TASAF | - | Tanzania Social Action Fund |
| TCB | - | Tanzania Commercial Bank |
| TCRA | - | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| TCU | - | Tanzania Commission for Universities |
| TDHS | - | Tanzania Demographic and Health Survey |
| TEHAMA | - | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UNSCR 1325 | - | United Nations Security Council Resolution 1325 |
| UNICEF | - | United Nations Children's Fund |
| UN Women | - | United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women |
| THIS | - | Tanzania HIV/AIDS Impact Survey |
| WEE | - | Women Economic Empowerment |
| WCF | - | Workers Compensation Fund |
| WDF | - | Women Developmend Fund |
| VICOBA | - | Village Community Bank |
| VSLA | - | Village Savings and Lending Associations |
| VTC | - | Vocational Training Centers |
| TDHS/MIS | - | Tanzania Demographic Health Survey/ Malaria Indicator Survey |

# TAFSIRI YA MANENO

Kwa madhumuni ya Sera hii, maneno yafuatayo yatatafsiriwa kama ifuatavyo: -

| | |
|---|---|
| Jinsi | Ni hali ya kimaumbile inayotofautisha mwanaume na mwanamke ambayo mtu huzaliwa nayo. Tofauti za kijinsi ni za kibaiolojia na hazibadiliki. |
| Jinsia | Mgawanyo wa majukumu baina ya wanawake na wanaume katika jamii. Mgawanyo huo unatokana na mitazamo iliyojengeka ndani ya jamii husika ambapomajukumu hayo yanaweza kutofautiana kulingana na muda au baina ya jamii moja na nyingine. |
| Majukumu ya Kijinsia | Majukumu tofauti kati ya wanawake na wanaume yaliyobainishwa na kuendelezwa kijamii kwa mfano, kupika, kufua, kuteka maji na kusafisha nyumba yanatambulika kama majukumu ya kijinsia ya wanawake badala ya kuwa ni majukumu ya wote. |
| Makundi Maalum | Makundi haya yanajumuisha Wazee, Wanawake, Watoto, Wajane, Wagumba, Wafanyabiashara ndogo ndogo na Watu Wenye Ulemavu. |
| Mlingano wa Kijinsia | Kipimo cha kitakwimu ambacho hutoa thamani ya nambari ya uwiano wa wanawake na wanaume au wasichana na wavulana kwa kutumia viashiria kama vile: mapato au elimu. Kwa mfano, mlingano wa kijinsia unaotokana na kuwepo kwa idadi sawa ya wasichana na wavulana waliomaliza elimu ya msingi, sekondari au vyuo. |
| Usawa wa Kijinsia | Ni hali ya kuwa na haki sawa kati ya wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, watoto wa kike na wa kiume. |
| Uwiano wa Kijinsia | Dhana ya haki na usawa katika mgawanyo wa rasilimali, faida na wajibu kati ya wanaume na wanawake, wasichana na wavulana katika nyanja zote za maisha. Katika kuhakikisha uwiano sawa, ni muhimu hatua chanya za muda mfupi au mrefu ziwekwe ili kufidia upungufu wa kihistoria na kijamii unaozuia wanawake kupata fursa sawa na wanaume. |
| Jitihada za Makusudi | Ni hatua zinazotoa kipaumbele kwa wanawake ili kurekebisha kutokuwepo kwa usawa katika kupata rasilimali, mamlaka au fursa mbalimbali. Ni dhamira ya dhati na ya muda inayowekwa kufidia hasara na mapengo ya kihistoria na kijamii yanayozuia ushiriki wa wanawake katika fursa mbalimbali. |
| Umaskini | Ni hali ya kuwa na uwezo duni wa kujikimu na ustawi. Hali hii inatokana na kukosekana kwa rasilimali au mapato toshelevu na hivyo kusababisha kukosekana kwa mahitaji ya msingi ya maisha kama vile lishe, afya bora, maji, malazi, mavazi na elimu. Pia, kuna umaskini wa muda unaowaathiri zaidi wanawake na wasichana kutokana na kuwepo kwa mila na desturi kandamizi na majukumu ya kijinsia ya kulea na kuhudumia familia na kaya yasiyokuwa na malipo. |
| Bajeti inayozingatia masuala ya Jinsia | Ni mgawanyo wa rasilimali unaojumuisha uchambuzi wa mapato na matumizi kwa mtazamo unaozingatia usawa na uwiano wa kijinsia. Aidha, matokeo ya utekelezaji wa bajeti inayozingatia mahitaji ya kijinsia yatakuwa na manufaa sawa kwa makundi yote. |

# DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua umuhimu wa kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake. Uwepo wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000 na Mkakati wa Utekelezaji wake ya Mwaka 2005 unathibitisha dhamira ya wazi ya Serikali ya kukuza usawa wa kijinsia kama njia mojawapo ya kuimarisha ustawi na maendeleo ya watu wake. Sera hiyo ilishughulikia tofauti kadhaa za kijinsia ili kuongeza ushiriki wa wanawake na wanaume katika kufikia maendeleo endelevu. Misingi elekezi ya Sera hiyo imetokana na Mikataba, Maazimio, Itifaki na Mipango ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa ambayo ni pamoja na: Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake - CEDAW (1979) na Itifaki yake ya Hiari; Azimio la Baraza la Usalama 1325 la mwaka 2000 kuhusu Amani na Usalama kwa Wanawake; Azimio la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) la Jinsia na Nyongeza yake ya Kuzuia na Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (1997); Azimio la Beijing na Jukwaa la Utekelezaji - BPfA (1995); Itifaki ya SADC ya Jinsia na Maendeleo (2008); na Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030).

Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000 umekuwa na mafanikio makubwa kama yalivyoelezwa katika sura zinazofuata. Hata hivyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Sera hiyo kumekuwa na mabadiliko makubwa duniani ikiwa ni pamoja na kukua kwa matumizi ya teknolojia, mabadiliko ya tabianchi na milipuko ya magonjwa mbalimbali yaliyoathiri maendeleo ya wanawake na wanaume kwa ujumla. Vilevile, upungufu wa kisera na masuala mapya ya kijinsia yaliyoibuka ambayo hayakuzingatiwa katika Sera hiyo na kusababisha kutofikia lengo lililokusudiwa. Hali hii ilionesha uhitaji wa kufanyika kwa Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000 ambayo ilibainisha upungufu katika utekelezaji wa masuala mapya kwa mrengo kwa kijinsia. Matokeo ya tathmini yaliweka msingi wa kufanya mapitio ya Sera na Mkakati wake wa Utekelezaji (2005) na hivyo kuweka msukumo wa kuandaliwa kwa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023.

Pamoja na masuala mengine yaliyojumuishwa, Sera hii imebainisha hatua za kimkakati za kukuza na kuharakisha kufikiwa kwa usawa wa kijinsia nchini. Hivyo, ni rai yangu kwa wadau wote zikiwemo Wizara za Kisekta, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo na jamii kwa ujumla, kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Matamko ya Sera hii ili kufikia usawa wa kijinsia, pamoja na kuhakikisha kuwa jamii ya Watanzania inaishi kwa umoja na mshikamano kati ya wanaume, wanawake, wasichana na wavulana na kuwa wote wanapata huduma za msingi na haki sawa.

Aidha, hatua za maandalizi ya Sera hii zimehusisha wadau wengi kutoka maeneo mbalimbali nchini. Hivyo, kwa niaba ya Serikali, ninawashukuru wadau wote kwa michango yao muhimu waliyoitoa katika hatua zote za kuandaa Sera hii ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023.

Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb.)
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,**
**WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SURA YA KWANZA
# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli

Kufikia usawa wa kijinsia ni suala linalokubalika ulimwenguni kote kama mkakati wa kimaendeleo wa kupunguza pengo la umaskini baina ya wanawake na wanaume, kuboresha hali za maisha na afya pamoja na kuboresha uwekezaji katika sekta ya umma na binafsi. Usawa wa kijinsia sio suala la haki za wanawake tu, bali ni suala linalohusu makundi mengine ikiwemo wanaume, vijana, watoto, wazee, wajane, wagumba, wafanyabiashara ndogondogo na watu wenye ulemavu. Pia, ni suala muhimu katika kuleta maendeleo jumuishi na endelevu. Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya Mwaka 2000 (Sera ya Mwaka 2000) ilitoa dira ya usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maendeleo ikiwemo elimu, afya, nafasi za maamuzi na uchumi. Sera hiyo iliweka mazingira wezeshi kwa wanawake na wanaume katika kutekeleza majukumu yao kulingana na mahitaji yao ya kijinsia.

Sera hiyo iliweka mikakati madhubuti ya kuwawezesha wanawake, wanaume na jamii kushiriki katika jitihada za kutokomeza umaskini; kuwawezesha wanawake na wanaume kutumia rasilimali zilizopo ili kujiletea maendeleo; kuiwezesha jamii kuzingatia haki na usawa baina yao na hivyo kuweka mazingira wezeshi ili kujiletea maendeleo; kuiwezesha jamii kutambua na kuthamini mchango wa wanawake katika maendeleo ya familia na Taifa na kuzilinda haki zao; na kuiwezesha jamii kutambua umuhimu wa ushiriki wa wazazi wote wawili katika malezi bora ya watoto. Sera hiyo pia iliweka mikakati ya kuendeleza viwanda ili kuchochea mageuzi na maendeleo ya kiuchumi, pamoja na kuonesha dhamira ya Serikali katika kuimarisha mfumo wa kisheria ili kufikia usawa wa kijinsia kwa kuzingatia na kuhakikisha haki sawa mbele ya sheria kwa makundi maalum wakiwemo wanawake.

Sera hiyo ilizingatia Mikataba, Maazimio na Mipango ya Kimataifa na Kikanda ambayo Tanzania iliridhia na kuitekeleza ili kuleta usawa wa kijinsia katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Mikataba, Maazimio na Mipango hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979); Mkataba wa Kuondoa Ubaguzi katika Ajira na Kazi (1958); Mkataba wa Kimataifa wa Idadi ya Watu na Maendeleo (1994); Mkataba wa Wafanyakazi wenye Majukumu ya Kifamilia (1981); Mkataba wa Haki ya Uzazi (2000); Malengo ya Maendeleo ya Milenia (2000) hususan lengo la 3 la Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake; Mkataba wa Kimataifa wa haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (1966); Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto (1989) ambao unalenga katika haki mahsusi za Mtoto; Mkataba wa Afrika kuhusu UKIMWI na Magonjwa ya Ngono (1999); Mkataba wa Wanawake unaohusu Utamaduni wa Amani wa Afrika ulioridhiwa Zanzibar (1999); Mkataba wa Kimataifa wa haki za Kiraia na Kisiasa (1966); Azimio la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (1948); Mkataba wa Haki za Kisiasa za Wanawake (1952); Mkataba wa Afrika wa Haki za Watu na Binadamu (1981); Azimio la Ulingo wa Beijing (1995); Azimio Namba 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa Kuhusu Amani na Usalama kwa Wanawake (2000); na Azimio la Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) la Jinsia na Nyongeza yake ya Kuzuia na Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto

(1997); Serikali katika jitihada za kuweka msukumo wa kutekeleza mikakati ya kuendeleza haki na usawa wa kiuchumi kwa wanawake, inatekeleza ahadi zake kwenye Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (2021) zenye lengo la kuongeza kasi ya utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing. Aidha, Tanzania inatekeleza Azimio namba 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kuhusu Amani na Usalama kwa Wanawake ambalo linataka nchi wanachama kuangalia usalama wa wanawake wakati wa migogoro ya kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Katika ngazi ya Kitaifa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa fursa sawa ya ushiriki wa wanawake na wanaume katika nyanja zote za maisha. Sura ya 3 Ibara ya 12(2) ya Katiba inatoa haki ya kuheshimiwa kama ilivyoainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu. Vilevile, Ibara ya 21 ya Katiba inasisitiza kuwa kila mtu ana haki ya kushiriki katika uongozi moja kwa moja au kwa njia ya uwakilishi, ambapo Ibara ya 22 inatoa fursa sawa za kushika madaraka ya umma. Kupitia marekebisho mbalimbali Katiba inaelekeza kufanya jitihada za makusudi (Affirmative Actions) ili kurekebisha upungufu uliokuwepo katika uwakilishi wa wanawake kwenye vyombo mbalimbali vya maamuzi kama vile Bunge na Mabaraza ya Madiwani kwa mabadiliko kupitia Sheria Na. 4/1992, 12/1995 na 3/2000. Vilevile, Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 inasisitiza kuhusu usawa wa kijinsia na kuondoa aina zote za ubaguzi na ukatili wa kijinsia nchini.

Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 imeonesha mafanikio mbalimbali yaliyopatikana na jitihada za Serikali za kuingiza masuala ya jinsia katika Sera, Mikakati, Programu, Sheria, Mipango na Bajeti zote za kisekta. Mafanikio hayo ni pamoja na: kupunguza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18 – 2021/22); kuanzishwa kwa Madawati ya Jinsia katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuweka msukumo wa kutunga sheria zinazozingatia masuala ya kijinsia na kufanya mapitio ya sheria kandamizi; kuanzisha programu za uwezeshaji wanawake kiuchumi; kutoa elimu bila ada kwa watoto wa kike na wa kiume hivyo kuongeza udahili katika shule za msingina sekondari ambapo kwa sasa uwiano wa udahili kwa watoto wa kike na wa kiume umefikia 1:1; nakuimarika kwa upatikanaji wa huduma za afya kwa wanawake hususan huduma za uzazi.

Mafanikio mengine ni pamoja na: kuanzishwa kwa programu mbalimbali za kupunguza umaskini kama vile Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ambazo zinazingatia usawa wa kijinsia hasa katika suala zima la kuinua uchumi kwa wanawake; Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF) ambao unatoa fursa kwa wanawake na wanaume walio kwenye sekta binafsi kupata huduma za bima ya afya; kuwepo kwa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) pamoja na mifuko mingine ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inayowezesha wanawake kupata mitaji; kuandaa na kutekeleza bajeti zinazozingatia masuala ya kijinsia (GRB) kuanzia ngazi ya jamii hadi Taifa ili kuhakikisha kuwa bajeti hizo zinawanufaisha wanawake, wanaume na makundi maalum; kutambua umuhimu wa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na hivyo kuchochea kufanyika kwa marekebisho ya Sheria ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 hususan kifungu kipya cha 37A kinachozitaka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kutenga asilimia 10 ya mapato yao ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya kiuchumi vya Wanawake (4%), Vijana (4%) na Watu wenye Ulemavu (2%); na kuongezeka kwa idadi ya wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi na

maamuzi katika ngazi zote.

Pamoja na mafanikio hayo, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 imebainisha upungufu na changamoto zilizoathiri utekelezaji wa Sera hiyo ikiwa ni pamoja na kutofikiwa kwa usawa wa kijinsia. Hali hii imethibitishwa na vipimo vya usawa wa kijinsia (Gender Inequality Index – GII na Social Institutions and Gender Index - SIGI) ambapo Tanzania imepata alama 0.539 (GII) na 0.262 (SIGI, 2022) ikiwa ni viwango vya chini vya kufikia usawa wa kijinsia. Tathmini pia ilionesha kuendelea kuwepo kwa mila na desturi kandamizi zinazowanyima wanawake fursa za kumiliki rasilimali; kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia; ushiriki mdogo wa wanaume katika jitihada za kuleta usawa wa kijinsia; na kuendelea kuwepo kwa vifo vinavyotokana na uzazi kutokana na mila na tamaduni zenye madhara. Vilevile, ongezeko la uzito wa kazi kwa wanawake unaosababishwa na upungufu wa upatikanaji wa huduma mbalimbali ikiwemo maji na nishati; na huduma za Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kutowafikia wanawake na wanaume walioko kwenye sekta isiyo rasmi.

Aidha, Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 imebainisha upungufu katika kutoa mwelekeo wa kisera katika maeneo mapya na muhimu ambayo yameibuka katika kipindi cha miongo miwili tangu kutungwa kwa Sera. Upungufu huo ni pamoja na: Sera kutojumuisha aina nyingine za ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili wa kisaikolojia, ukatili kwa njia ya TEHAMA hususan katika mitandao ya kijamii, ukatili wa kimwili na kingono ikiwemo unyanyasaji wa kingono kwenye Taasisi za Elimu; kutokuwepo kwa msukumo wa uzingatiwa wa masuala ya jinsia na afya hususan uhimizaji wa wanawake, wasichana, wanaume na wavulana kuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ikiwemo magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume; usalama na amani kwa wanawake; jinsia na huduma za kidijitali. Vilevile, Sera haikuzingatia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora na VVU/UKIMWI hivyo kukosa matamko ya kisera.

Vilevile, Sera ya Mwaka 2000 haikujumuisha baadhi ya Mikataba, Maazimio na Mipango ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa inayohusu usawa wa kijinsia ambayo iliridhiwa baada ya mwaka 2000. Nyenzo hizo ni pamoja na Azimio Na. 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2000) kuhusu Amani na Usalama kwa Wanawake ambalo linazitaka nchi wanachama kuangalia usalama wa wanawake wakati wa ulinzi wa amani, migogoro ya kisiasa, kiuchumi na kijamii; Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Genaration Equality Forum - 2021) lenye maeneo sita ya utekelezaji ambapo Tanzania imechagua eneo la pili la Haki na Usawa wa Kiuchumi ambalo pamoja na mambo mengine linahimiza umuhimu wa kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake kwa kuanzisha na kuendeleza vituo vya malezi na makuzi ya awali ya watoto vya jamii na ushiriki wao kwenye shughuli za kiuchumi; Itifaki ya SADC ya Jinsia na Maendeleo (2008) Ibara ya 10 - haki za wajane na Ibara ya 12 – uwiano sawa katika nafasi za maamuzi na uongozi kwenye sekta ya umma na binafsi (50:50); Itifaki ya Haki za Wanawake Barani Afrika (2003), Ibara ya 10 – 11 kuhusu ulinzi na ushiriki wa wanawake katika amani na usalama, pia Ibara ya 19 – haki za wajane; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 (SDGs) hususan lengo la tano, Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063) lengo la 17 kuhusu usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha; na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 unaoelekeza ujumuishaji wa makundi maalum ikiwemo wanawake katika masuala ya kifedha.

## 1.2 Hali ilivyo katika Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000

Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 umekuwa na mafanikio katika kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mafanikio yaliyopatikana yametokana na ushirikiano kati ya Serikali na wadau mbalimbali wakiwemo Wabia wa Maendeleo, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia na Jamii kwa ujumla. Hivyo, kipengele hiki kinabainisha hali ilivyo katika utekelezaji wa masuala ya jinsia na maendeleo ya wanawake, mafanikio, upungufu na changamoto.

### 1.2.1 Utekelezaji wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake

Tathmini ya utekelezaji imezingatia maeneo ya msingi ya Sera ya Mwaka 2000 kama ifuatavyo:-

#### 1.2.1.1 Hali ya Wanawake Kiuchumi

Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 ulihusisha jitihada za kisera, kisheria na mikakati iliyolenga kuwawezesha wanawake kiuchumi kama njia mahsusi ya kukuza uchumi nchini. Jitihada hizo ni pamoja na: Mabadiliko katika Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290 hususan kifungu 37A ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani (Wanawake 4%, Vijana 4% na Watu wenye Ulemavu 2%) ili kutoa mikopo isiyo na riba kwa wajasiriamali ambapo hadi kufikia Juni, 2022 jumla ya Shilingi Bilioni 111.03 zilitolewa kwa vikundi vya wanawake 34,505.

Vilevile, kuanzishwa kwa Benki ya Wanawake Tanzania ambayo ilikuwa ni Benki ya mfano kwa nchi za Afrika ambapo kutokana na mabadiliko ya kiuendeshaji majukumu Benki hiyo yalihamishiwakatika Dirisha la Wanawake katika Benki ya Biashara Tanzania (TCB). Katika kipindi cha 2018/19 hadi 2021/22, jumla ya kiasi cha Shilingi Bilioni 62.55 kilitolewa kwa wanawake wajasiriamali 18,125katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara kupitia Dirisha hilo. Aidha, Sera ilitoa msukumo wa kuimarisha usimamizi wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake unaotoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali ili kukuza miradi na biashara zao. Pia, Sera hiyo imechagiza uanzishwaji wa madirisha mahsusi ya kutoa mikopo kwa wanawake katika benki za biashara nchini,ikiwemo Tabasamu (TCB), Fanikisha, Wewe ni Jasiri (Azania Benki), Jasiri Bond (NMB), Malkia (CRDB), Johari (NBC) na Fanikisha (Equity Bank). Mfano, NMB hadi kufika mwaka 2021/22 kupitiaJasiri Bond imewezesha kiasi cha shilingi Bilioni 288.33 kwa wanawake 10,565. Mikopo hii imesaidiawanawake wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza biashara na shughuli nyingine za uzalishaji na hivyo kupunguza hali ya utegemezi.

Sera ya Mwaka 2000 imechangia katika kuweka mazingira wezeshi kwa kutambua, kusajili na kuhamasisha Vikundi vya Kijamii vya kuweka na kukopa vikiwemo ASCAs, VSLA, VICOBA, SACAs na SACCOs mijini na vijijini ili kuwasaidia wananchi ambao hawana sifa za kukopesheka kwenye Taasisi rasmi za Fedha. Vilevile, Serikali imetenga maeneo maalum yenye jumla ya ekari 15,822.64 katika Halmashauri 150 kwa ajili ya kufanyia biashara. Sambamba na hilo, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 imerekebishwa kwa kuelekeza Taasisi za Umma kutenga asilimia 30 ya thamani ya manunuzi kwa wanawake.

Mafanikio mengine ni pamoja na: kuandaliwa kwa Mfumo Jumuishi wa Fedha wa Pili (Financial Inclusion Framework 2023 - 2027) ambao unatoa kipaumbele katika kutatua changamoto za kifedha kwa makundi yasiyofikiwa na mifumo rasmi ya kifedha ambayo wengi wao ni wanawake; kuimarika kwa upatikanaji wa masoko ya bidhaa za wanawake wajasiriamali kupitia kushiriki kwenyemaonesho ya biashara ndani na nje ya nchi kama vile Nanenane, Sabasaba na Juakali ambapo idadi ya wanawake walioshiriki imeongezaka kutoka 268 mwaka 2010 mpaka 13,566 mwaka 2020.Aidha, imewezesha vijana 812 kushiriki katika kilimo biashara (kati yao Wanawake ni 282 sawana asilimia 34.73 na wanaume 530 sawa na asilimia 65.27) kupitia programu ya Building Better Tomorrow: Youth Initiative in Agribusiness (BBT-YIA).

Pamoja na mafanikio hayo, wanawake wengi bado wapo kwenye mifumo isiyo rasmi na hawafikiwi na fursa za kiuchumi kutokana na mifumo ya kifedha kutokuzingatia mahitaji ya kijinsia. Hiiinatokana na ukweli kuwa, wanawake wengi hawamiliki rasilimali kama ardhi ambayo ingetumika kama dhamana ya mikopo. Hivyo, ni muhimu kwa Serikali na wadau wote kuongeza jitihada katika kuongeza usimamizi wa mifumo ya fedha na fursa za kibiashara ili kuhakikisha wanawake na wanaume wanakuwa na haki sawa katika kumiliki na kutumia rasilimali zilizopo.

### 1.2.1.2 Mikakati ya Matumizi Bora ya Rasilimali na Nyenzo

Sera ya Mwaka 2000 ilitoa kipaumbele katika eneo la upatikanaji, umiliki na utumiaji wa ardhi kwa usawa baina ya wanawake na wanaume na kuendeleza matumizi ya ardhi ya kilimo vijijini, kuimarisha vitendea kazi, masoko na mawasiliano/miundombinu ya usafirishaji wa mazao vijijini.

Ili kuhakikisha kuwa umiliki wa ardhi unazingatia usawa wa kijinsia, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali zikiwemo utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi (2000), Sera ya Taifa ya Ardhi (1995), Marekebisho ya mwaka 2017 ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura ya 114 kifungu cha3 (2) yanatoa fursa kwa kila mwanamke kumiliki na kutumia ardhi pamoja na kuanzisha Kamati za kuhamasisha haki za wanawake kumiliki ardhi. Jitihada hizi zimewezesha kuongezeka kwa idadi ya wanawake wanaomiliki ardhi kutoka asilimia 9 ya hapo awali hadi kufikia asilimia 25 mwaka 2018 na kuongezeka kwa umiliki wa pamoja kutoka asilimia 6 hadi asilimia 16 mwaka 2018. Hadi Aprili, 2023, jumla ya Hatimiliki za kimila 39,023 zilitolewa ambapo kati ya hizo Hatimiliki za kimila 13,008 sawa na asilimia 33.3 zilizotolewa kwa wanawake na 26,015 zilitolewa kwa wanaume. Aidha, wanawake 15,102 walipatiwa Hatimiliki kati ya Hatimiliki 45,306 zilizotolewa.

Mafanikio mengine ni kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika sekta ya Ardhi inayowezesha upatikanaji wa Hatimiliki za kietroniki zinatolewa kwa kuzingatia jinsia. Pamoja na jitihada hizo bado umiliki wa ardhi kwa wanawake umeendelea kuwa ni changamoto kutokana na mila na desturi hasi pamoja na mifumo ya kisheria hususan za kimila zinazotoa mianya ya ubaguzi wa kijinsia katika umiliki wa ardhi, hivyo msukumo wa makusudi unahitajika katika kuleta haki na usawa wa kumiliki ardhi kwa wanawake na wanaume. Kwa mujibu wa utafiti wa SIGI (2022) wanawake asilimia 26 tu wanamiliki ardhi ya kilimo. Hali hii inatokana na kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zinazowapendelea wanaume kurithi na kumiliki ardhi ya familia.

Utekelezaji wa Sera hiyo uliweka mkazo katika kuongeza ushiriki wa wanawake hususan wanaoishi vijijini katika kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa. Kutokana na kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia miongoni mwa jamii, wanawake wamekuwa na fursa finyu hususan ya kuwekeza kwenye kilimo cha mazao yenye thamani kubwa. Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa asilimia zaidi ya 80 ya wanawake waishio vijijini hutumia muda wao mwingi kwenye shughuli za Kilimo, huku wakitumia saa 4 hadi 5 zaidi ya wanaume katika shughuli za uzalishaji mali hasa mashambani lakini wamekuwa hawanufaiki na mali wanazozalisha. Aidha, uwezo wa wanawake kumiliki rasilimali za uzalishaji kama vile ardhi ni mdogo. Hivyo, wanawake wakulima humiliki wastani wa asilimia 40 tu ya ukubwa wa shamba ambayo huzalisha mazao kidogo. Matokeo ya utafiti wa Sensa ya Kilimo iliyofanyika 2019/20 yanaonesha kuwa kati ya kaya 12,007,839 Tanzania, kaya 7,837,405 (65.3%) zinajihusisha na shughuli za kilimo. Kwa upande wa Tanzania bara, kati ya kaya 7,657,185 zinazojihusisha na kilimo, kaya 4,972,372 (64.9%) zinalima mazao, kaya 2,526,846 (33%) mazao na ufugaji na kaya 157,290 (2%) zinajishughulisha na ufugaji pekee.

Pamoja na jitihada zilizofanyika katika kuimarisha Sekta ya Kilimo na kuleta ushiriki sawa wa wanawake na wanaume, bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi zinazosabisha kuwa na uzalishaji mdogo; matumizi ya teknolojia duni za kilimo hususan kwa wakulima wanawake; ujuzi mdogo kwa wakulima; na ukosefu wa masoko ya uhakika na taarifa sahihi za bei za mazao.

Katika muktadha huo, upo uhitaji wa kuhamasisha masuala ya kijinsia katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanapata haki sawa. Uboreshaji wa miundombinu ya kilimo vijijini (barabara, miundombinu ya umwagiliaji na mifumo ya TEHAMA) unapaswa kuimarishwa ili kuongeza tija kwa wakulima wa vijijini na kuboresha usalama wa chakula na lishe. Upo umuhimu wa kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha ikiwemo mikopo na ujuzi wa usimamizi wa kifedha kwa wakulima wanawake wa vijijini ili kutoa fursa zaidi za uwekezaji wao katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, hivyo kuongeza ajira na kipato.

#### 1.2.1.3 Mila na Desturi

Nchini Tanzania, zipo mila na desturi nzuri katika jamii zinazofaa kuendelezwa mfano mila zinazohamasisha uhifadhi wa mazingira na uoto wa asili kwa kuzuia uharibifu kwenye maeneo kama vile misitu, vyanzo vya maji na milima ambayo jamii iliaminikuwa miungu yao inaishi hapo. Aidha, katika malezi ya mtoto ilijengeka kuwa mtoto ni wa wote na kila mwanajamii anajukumu la kumlea. Hata hivyo, zipo baadhi ya mila na desturi ambazo ni kandamizi kwa wanawake katika ngaziya familia, ukoo na jamii kwa ujumla. Mila hizo ni pamoja na: ndoa za utotoni, kurithi na kutakasa wajane; wanawake kutokumiliki au kurithi rasilimali za uzalishaji, ukeketaji na unyago. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera jitihada mbalimbali zimefanyika kama ifuatavyo:-

##### 1.2.1.3.1 Ukeketaji

Kwa mujibu wa Utafiti wa SIGI (2022), asilimia 12 ya wanawake nchini Tanzania wamekeketwa. Mikoa inayoongoza kwa ukeketaji ni Arusha (63%) ukifuatiwa na Manyara (58%). Pia, maeneo ya vijijini asilimia 15 yameonesha kuwa na hali ya ukeketaji mara mbili zaidi ya maeneo ya mijini asilimia 7. Aidha, Wanawake na wasichana waliofanyiwa ukeketaji kwa mujibu wa tafiti za UNICEF (2013)

nchini Tanzania ni milioni 7.9 na TDHS/MIS(2015-16) ni asilimia 10. Matokeo ya utekelezaji wa Sera hiyo ni pamoja na kuandaliwa kwa Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kutokomeza Ukeketaji nchini (2020/21 - 2024/25); kufanyika kwa kampeni za kutoa elimu na ushawishi kwa makundi mbalimbali kuhusu kutokomeza ukeketaji na kuanzishwa kwa nyumba salama 11 kwa ajili ya kuwatunza manusura wa ukatili ikiwemo ukeketaji.

### 1.2.1.3.2 Ndoa za Utotoni

Sera ya Mwaka 2000 ililenga pia kutokomeza ndoa za utotoni kwa kuandaa na kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA, 2017/18 – 2021/22) ili kuzuia aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto zikiwemo ndoa za utotoni; kuzijengea jamii uelewa juu ya madhara ya ndoa na mimba za utotoni; kutungwa kwa Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 ili kulinda haki na ustawi wa mtoto pamoja na marekebisho ya Mwaka 2015 ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 ikisomwa pamoja na Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 ambazo zinaweka katazo la ndoa na mimba kwa watoto hususan wanafunzi; Kutungwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 inayotoa msaada wa kisheria kwa wasio na uwezo wa kugharamia huduma za kisheria na ada za utetezi kwa makundi maalum wakiwemo wanawake na watoto.

Jitihada hizo zimewezesha kupatikana kwa mafanikio ikiwa ni pamoja na: uanzishwaji wa Kamati za Ulinzi za Wanawake na Watoto 18,186 unaojumuisha kamati katika ngazi ya Taifa (2), Mikoa (26), Halmashauri (148), Kata (3,501), Vijiji (10,507), na Mitaa (4,002) zinazoshughulikia masuala ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; kuanzishwa kwa mifumo ya kuzuia ndoa za utotoni katika ngazi za chini ambazo ni pamoja na Mabaraza ya Watoto 1,669 katika ngazi zote na Klabu za Watoto 2,552 katika shule za Msingi na Sekondari; kutekeleza Sera ya Elimu bila malipo kuanzia shule za awali hadi kidato cha sita kwa shule za umma; adhabu ya kifungo cha kuanzia miaka 30 jela kwa yeyote anayepatikana na hatia ya kuoa au kumpa mwanafunzi mimba; kuanzishwa kwa huduma ya simu bure kwa watoto (Child Help Line namba 116) ili kutoa huduma saidizi kwa Watoto manusura na walio katika hatari ya kufanyiwa ukatili; kujengwa nyumba salama 11 ili kutoa hifadhi kwa manusura wa ukatili; na kuanzishwa kwa mahakama za watoto 141 kwa ajili ya kuimarisha mfumo wa mahakama juu ya masuala ya ukatili dhidi ya watoto. Aidha, uandaaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008); marekebisho ya Fomu ya Polisi Na.3 (PF.3) na mwongozo wa kujaza PF.3 ni miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana. Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi Tanzania limeimarisha mwitikio wa kesi za ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa kuanzisha Mtandao wa Polisi Wanawake pamoja na kutoa mafunzo kwa maafisa wa jeshi hilo kuhusu mbinu za kuwahudumia manusura wa ukatili nchini.

Pamoja na jitihada kubwa za kushughulikia tatizo la ndoa za utotoni nchini, matukio haya yanaendelea kufanyika katika maeneo mengi. Kwa mujibu wa Taarifa ya SIGI (2022) asilimia 19 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 na zaidi na asilimia 16 ya wanawake wenye umri wa miaka 20 hadi 24 waliolewa kabla ya umri wa miaka 18. Aidha, kwa mujibu wa Takwimu za Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani za Jeshi la Polisi kwa mwezi Januari hadi Mei, 2022, Mikoa inayoongoza kwa matukio ya wanafunzi kupata mimba ni Shinyanga (matukio 82), Mwanza (matukio 79) na Arusha (matukio 71). Hali hii inatoa msukumo wa kuchambua upungufu katika mifumo ya kisera na kisheria iliyopo ili kudhibiti ukiukwaji wa haki za watoto ikiwemo mimba za utotoni kwani huwanyima watoto wa kike fursa za kujiendeleza kielimu na hata kiuchumi.

#### 1.2.1.4 Jinsia na Afya ya Uzazi

Sera ya Mwaka 2000 ililenga katika kutekeleza malengo matatu (3) yakiwemo kuendeleza teknolojia ya uhakika wa chakula, kuimarisha programu ya mafunzo ya lishe bora kwa wanawake na jamii kama njia ya kinga na magonjwa, kila familia kuhakikisha inahifadhi chakula cha kutosha na kuuza ziada tu. Sera pia iliainisha baadhi ya athari zinazoweza kutokea ikiwemo kudumaa, upungufu wa damu na kuzaa watoto njiti; maradhi na vifo kutokana na magojwa kama vile VVU/UKIMWI au kupoteza damu nyingi wakati wa uzazi na wakati wa kukeketwa. Mafanikio ya utekelezaji wa sera katika eneo hili ni pamoja na kuandaliwa kwa miongozo ya kushughulikia tatizo la utapiamlo, ikiwemo udumavu, upungufu wa damu na uzazi wa watoto njiti; kuandaliwa na kutelezwa kwa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Lishe (National Multisectoral Nutrition Action Plan II – NMNAP II 2021/22 – 2025/26) unaotekelezwa na Halmashauri zote nchini ambao umeongeza uwajibikaji wa afua za lishe; kutengwa kwa shilingi 1,000 kwa kila mtoto kwa Halmashauri zote za kutekeleza afua za lisheikiwemo kutoa elimu kwa ngazi ya wataalam na jamii, matone na vitamini A na kuongeza damu kwamama wajawazito; Kuwepo kwa kampeni za kuelimisha jamii kuhusu tatizo la udumavu, upungufu wa damu na kuzaa watoto njiti.

Vilevile, huduma bila malipo kwa wajawazito na watoto walio na umri chini ya miaka mitano pamoja na wazee zimeendelea kutolewa. Katika kuboresha huduma za uzazi, Sera ya Afya ya Taifa (2007) inaelekeza kuwa wajawazito wapate huduma ya afya ya uzazi angalau mara nne kabla ya kujifungua. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuwepo kwa vituo vya afya 1,360 vyenye uwezo wa kutoa huduma za uzazi pamoja na vifaa vya dharura. Kwa mujibu wa takwimu za afya kwa mwaka 2022, Tanzania ina vituo vya huduma za afya 9,104 Tanzania Bara vikiwemo vituo 52 vya kujifungulia/kulelea watoto. Takwimu za NBS zinaonesha uwiano kati ya watoto wanaozaliwa nchini na wataalam wa afya waliopo umeongezeka kutoka asilimia 59.3 (2008/09) hadi asilimia 69.6 (2014/15). Kutokana na jitihada hizi, utafiti uliofanywa na NBS, (TDHS-MIS, 2015/16) umeonesha kuwa asilimia 98.4 ya wanawake waliojifungua katika kipindi cha miaka mitano iliyopita walipokea baadhi ya huduma za uzazi kutoka kwa wataalam wa afya.

Tathmini ya Sera ya Mwaka 2000 ilibaini changamoto hususan ya wanawake kutofikia huduma za kiuchunguzi na kumudu gharama za afya ikiwemo uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na matiti na tatizo la afya ya akili. Mfano, mwaka 2015 wanawake waliofanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi walikuwa 127,188 ikilinganishwa na wanawake 513,375 mwaka 2022.

#### 1.2.1.5 Wanawake na Mazingira

Sera ya Mwaka 2000 ilijielekeza katika kuongeza uwiano wa ushiriki wa wanawake katika kamati za mazingira huku ikitambua athari za uharibifu wa mazingira, ikiwemo uzalishaji mdogo wa mazaona kuwaongezea mzigo wa kazi wanawake kwa kutembea mwendo mrefu kutafuta maji, kuni na malisho. Tathmini ya Utekelezaji wa Sera imebaini uwepo wa uwiano mzuri wa kijinsia katika kamati za hifadhi ya Mazingira ambapo theluthi moja (1/3) ya wajumbe ni wanawake katika ngazi ya Kata. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kutungwa kwa Sera, Mikakati Programu, Mipango, Sheria na Miongozo mbalimbali inayolenga kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira (2021); Sera ya Taifa ya Nishati (2015); Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2021 - 2026); Kanuni na Mwongozo wa Kitaifa wa Udhibiti na Usimamizi

wa Biashara ya Kaboni (2022); Programu ya Kilimo kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi (2015 - 2025); Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Mazingira (2022 - 2032); Sheria ya Misitu, Sura ya 323; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191; Sheria ya Nishati Vijijini ya mwaka 2005; Kanuni za Misitu (2004); Mkakati wa Kitaifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2012 - 2018); Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (2021 – 2026) na Mwongozo wa Kuingiza Masuala ya Jinsia katika Sera, Mikakati, Programu, Mipango, Miongozo na Bajeti za Kukabiliana na Mabadilikoya Tabianchi (2014).

Vilevile, Sera hizo zimechangia kuongezeka kwa afua za uhifadhi wa mazingira ambazo zimeonesha ushiriki wa wanawake katika utekelezaji. Mfano, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia (EBBAR) jumla ya walengwa 346 kati yao wanawake ni 187; Mradi wa majaribio wa kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria (ACC-LVBC) yenye jumla ya walengwa 355 kati yao wanawake ni 183; Mradi wa usimamizi endelevu wa ardhi katika Bonde la Ziwa Nyasa (SLM) yenye jumla ya walengwa 375 kati yao wanawake ni 188; Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bionuai (SLR) jumla ya walengwa 1,361 kati ya hao wanawake ni 416. Pamoja na mafanikio haya kuna umuhimu wa kuendeleza jitihada za pamoja ili kuhakikisha kuwepo kwa mifumo ya kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika sekta ya mazingira.

### 1.2.1.6 Hali ya Elimu na Mafunzo

Sera ya Mwaka 2000 ililenga katika kushughulikia upungufu uliokuwepo ili kuongeza ushiriki wa wasichana katika elimu. Upungufu huo ni udahili mdogo, mdondoko (drop out), Mitaala kutozingatia masuala ya kijinsia, ushiriki mdogo wa wasichana katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati, elimu kwa wazazi kuhusu umuhimu wa kusomesha watoto wa kike na kuimarisha elimu kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Sera imehamasisha ujenzi wa Shule za Msingi na Sekondari zikiwemo shule za bweni ili kupunguza kasi ya mdondoko (drop out) kwa wanafunzi hususan wa kike ambapo kati ya mwaka 2015 na 2021 shule za msingi ziliongezeka kutoka 16,899 hadi 18,546 na shule za sekondari kutoka 4,708 hadi 5,289. Jitihada nyingine ni pamoja na kuimarisha mfumo wa elimu nchini ili kuzingatia masuala ya kijinsia katika mitaala, vitabu vya kiada na ziada pamoja na mbinu za kufundishia na kujifunzia. Katika kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi wa kike shuleni na kuongeza kiwango cha ufaulu, Serikali imeendelea na jitihada za kujenga miundombinu rafiki ikiwemo ujenzi wa mabweni katika shule za sekondari, vyumba vya kujisitiri, vyoo na uboreshaji wa huduma ya maji. Vilevile, katika kupunguza mdondoko wa wanafunzi, Sera imechangia katika utekelezaji wa sheria zinazozuia ubaguzi na kuwalinda wasichana kwa kufanya marekebisho ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 inayopiga marufuku ndoa kwa wanafunzi wa shule ya msingi au sekondari. Sheria hiyo, pia inatoa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka 30 jela kwa mwanaume atakayempa mimba mwanafunzi na miaka mitano (5) jela kwa mtu yeyote atakayesaidia au kushawishi msichana wa shule ya msingi au sekondari kuolewa akiwa masomoni.

Kutokana na jitihada hizo, kumekuwa na ongezeko la udahili wa wasichana katika Elimu ya Msingi (darasa la I – VII) kutoka 8,298,377 (wasichana 4,218,377 na wavulana 4,079,905) mwaka 2015 hadi kufikia 11,196,788 (wasichana 5,639,081 na wavulana 5,557,707) mwaka 2021. Katika elimu ya Sekondari, idadi ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha 1 - 6 iliongezeka kutoka wanafunzi 1,774,383 (wasichana 953,394 na wavulana 871,410) mwaka 2015 hadi wanafunzi 2,671,927 (wasichana 1,389,613 na wavulana 1,282,314) mwaka 2021 (BEST, 2021). Kwa ujumla, Idadi ya wanafunzi wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu imeongezeka kutoka 213,829 (Wanawake 83,844 na Wanaume 129,985) Mwaka 2017/18 hadi 295,919 (Wanawake 130,030 na Wanaume 165,889) Mwaka 2021/22.

Jitihada nyingine ni kuimarishwa kwa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) yenye vyuo 42 na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) 55 ili kuweka mazingira wezeshi na fursa kwa wasichana na wavulana walio katika umri balehe na wanaokosa fursa za kuendelea na masomo katika mfumo rasmi. Kupitia mradi wa Ukuzaji wa Ujuzi Mbadala wa Kujifunza - ALSD mwaka 2022, jumla ya wanafunzi wa kike 3,333 walipata elimu baada kubainika kuacha shule au kutoandikishwa shule kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu - HESLB imeboresha upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wa kike wakiwemo wenye ulemavu na yatima kutoka familia maskini. Katika kipindi cha 2014/15 na 2019/20, jumla ya wanafunzi 717,710 walinufaika na mkopo ambapo asilimia 51.5 ni wanafunzi wa kike.

Kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa (2021), idadi ya wasichana waliohitimu mafunzo ya ufundi stadi ni 49,591 na wavulana187,589. Vilevile, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ilidahili wanafunzi 539 (wanaume 355 na wanawake 184) mwaka 2021 wakati mwaka 2020 ilidahili wanafunzi 722 (wanaume 472 na wanawake 250). Pia, katika mwaka 2021 Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 6,779 (wanaume 5,275 na wanawake 1,504) na mwaka 2020 chuo hicho kilidahili wanafunzi 6,137 (wanaume 4,764 na wanawake 1,373). Aidha, mwaka 2021 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 3,581 (wanaume 2,839 na wanawake 742) wakati mwaka 2020 wanafunzi 2,190 walidahiliwa (wanaume 1,537 na wanawake 653).

Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuwezesha wasichana wengi kujiunga na masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kwa kuimarisha maandalizi ya watoto wakiwa katika ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na vyuo. Serikali imejenga shule 10 za wasichana za masomo ya sayansi (kidato cha 5 na 6). Aidha, wanafunzi 1,338,884 walihitimu masomo ya STEM ambapo kati yao asilimia 41.8 ni wasichana. Vilevile, wasichana 244 wenye ufaulu wa juu wamefadhiliwa kusoma masomo ya utabibu, uhandisi, sayansi na teknolojia kupita Mfuko wa Ufadhili wa Samia (Samia Scholarship) kwa mwaka wa masomo 2022/23. Hata hivyo, ushiriki wa wasichana katika ngazi ya elimu ya juu pamoja na masomo ya STEM bado ni mdogo ikilinganishwa na idadi ya wanaume. Kwa mfano, mwaka 2020/21, wanafunzi katika vyuo vikuu nchini walikuwa 206,305 kati ya hao wanawake 88,667 na wanaume 117,638.

Changamoto nyingine ni kuendelea kuwepo kwa mdondoko wa wanafunzi wa kike. Kulingana na Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (2021) wanafunzi wa kike takriban

3,000 waliacha shule kwa sababu mbalimbali zikiwemo ndoa na mimba za utotoni, kukosekana kwa miundombinu inayozingatia masuala ya kijinsia shuleni, mila na desturi hasi zinazomnyima mtoto wa kike fursa ya elimu. Hivyo, jitihada za makusudi zinahitajika katika kuendelea kutatua changamoto hizo ili kuongeza kasi ya kuleta usawa wa kijinsia katika elimu.

#### 1.2.1.7 Kazi na Ajira

Sera ya Mwaka 2000 iliweka msisitizo katika kukuza usawa wa kijinsia kwenye eneo la ajira hususan kuwepo kwa takwimu sahihi za wanawake na wanaume katika ngazi zote na kuwepo kwa utaratibu maalum wenye urasimu mdogo katika utoaji wa leseni kwa wafanyabiashara ndogondogo. Jitihada mbalimbali zilizofanyika ni pamoja na uandaaji wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma (2008); na kujumuishwa kwa vifungu muhimu katika MKUKUTA II (2005 - 2010) ambavyo vilitambua kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika ajira. Vilevile, Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu (2010/11– 2025/26) unaotekelezwa kwa vipindi tofauti vya miaka mitano (5) wenye lengo mahsusi la kuongeza kasi ya ukuaji jumuishi wa uchumi na kupunguza umaskini kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji na kutengeneza ajira kwa vijana na makundi maalum wakiwemo wanawake.

Juhudi nyingine ni kutungwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298 na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 ambazo zinalenga kuimarisha usawa wa kijinsia sehemu za kazi. Vilevile, Sera ilichangia katika kutengeneza Mwongozo wa Ujumuishaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma unaolenga kuleta ufanisi mahali pa kazi na kuweka mazingira wezeshi yanayozingatia mahitaji ya kijinsia ikiwemo kujenga sehemu maalum kwa ajili ya kunyonyesha watoto. Pia, Serikali katika kukuza fursa za ajira inatekeleza Programu ya Kuzalisha Fursa za Ajira Nchini (2021), Mkakati wa Kukuza Ajira wa Mwaka 2008; kuchochea ukuaji wa Sekta Binafsi kama njia ya kuongeza ajira na kujiajiri pamoja na kuongeza uwekezaji katika sekta ya ujenzi na sekta nyingine zinazotoa ajira nyingi nchini ikiwemo sekta ya kilimo, utalii, madini na viwanda.

Pamoja na juhudi hizo, Tanzania ina wanawake wachache kuliko wanaume katika sekta ambazo zina uwezekano wa kuwa rasmi (NBS, 2018). Asilimia 51 ya wanawake wanafanya kazi katika sekta zisizo rasmi zinazoendesha biashara ndogondogo ikilinganishwa na asilimia 49 ya wanaume. Katika Sekta hizo, ujira wa wafanyakazi ni mdogo na hutolewa kila siku.

Utafiti uliofanywa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuhusu Utafiti wa Watu wenye Uwezo wa Kufanya Kazi Tanzania (ILFS) ya mwaka 2021 umebaini kuwa Sekta ya Umma imeajiri jumla ya watu 529,557 ambapo wanaume ni 301,266 ikiwa ni sawa na asilimia 56.9 wakati wanawake ni 228,291 sawa na asilimia 43.1 ikifuatiwa na sekta binafsi asilimia 72 wanaume na asilimia 28 wanawake. Hii inaonesha kuwa, wanawake wengi wanajishughulisha na ajira zisizo rasmi na zenye ujira mdogo ikilinganishwa na wanaume. Aidha, utafiti huo umebaini wanawake walio wengi wanajishughulisha na ajira zisizo salama na zenye ujira mdogo ikilinganishwa na wanaume. Pia, Utafiti huo unaonesha kuwa wanaume wana kipato kikubwa cha kila mwezi kuliko wanawake kwa wastani na katika aina zote za ajira ikihusisha kazi zenye ujira, ajira binafsi na katika sekta ya kilimo. Jumla ya mapato ya kila mwezi ni shilingi 390,992 ambapo wastani wa pato la wanaume kwa mwezi ni shilingi 396,885 ikilinganishwa na shilingi 378,469 kwa wanawake.

Changamoto zinazoendelea kukwamisha jitihada za Serikali na wadau katika kufikia usawa wa kijinsia katika ajira ni pamoja na:- kuendelea kuwepo kwa mifumo dume katika jamii, kuwepo kwa vitendo vya rushwa ya ngono; mitazamo hasi kutoka kwa waajiri kuhusu uwajibikaji wa mwanamke hususan kutokana na majukumu ya kifamilia na kibaiolojia, mtazamo hasi juu ya mgawanyo wa kazi na majukumu kati ya mwanamke na mwanaume; mtazamo hasi juu ya ushiriki wa wanawake na wanaume katika kada mbalimbali na baadhi ya wanawake kutokujiamini katika kutafuta fursa zaajira.

### 1.2.1.8 Hali ya Wanawake katika kufanya Maamuzi

Sera ya Mwaka 2000 iliweka msisitizo katika kuhakikisha kuwa mchango wa wanawake katika maendeleo ya Taifa unatambuliwa na kuthaminiwa, kuhakikisha kuwa wanawake na wanaume wanachangia kikamilifu katika jitihada za maendeleo, kuhamasisha takwimu za wanawake na wanaume katika kila ngazi ya uongozi zinaonekana bayana na rasilimali zigawiwe kwa kuzingatia jinsia, kuhamasisha wanawake na wanaume washirikishwe katika kupanga na kusimamia matumizi ya bajeti ya taifa.

Serikali imefanya juhudi za makusudi kutambua na kuthamini mchango wa wanawake katika ngazi za uongozi na maamuzi kwa kutenga nafasi za viti maalum kwa wanawake katika Bunge asilimia 30 na Mamlaka za Serikali za Mitaa asilimia 33. Jitihada hizo pia zimewekwa kwenye kamati mbalimbali za kiutendaji katika ngazi za Vijiji, Kata na Halmashauri. Kamati hizo ni kama vile kamati za maji, mazingira na ardhi ambazo zinahitaji uwakilishi wa wanawake angalau theluthi moja. Jitihada nyingine ni pamoja na uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika Mkakati wa Kijinsia wa Tume ya Uchaguzi Tanzania unaohakikisha usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake katika kipindi chote cha uchaguzi. Aidha, uwepo wa Mkakati na Mpango Kazi wa 2018-2021 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambao pamoja na masuala mengine unakuza ushiriki wa wanawake katika uongozi na siasa ambapo kipaumbele chake ni kujumuisha jinsia katika shughuli zote za Bunge. Vilevile Serikali ilianzisha Taasisi ya Uongozi mwaka 2011 ambapo pamoja na mambo mengine ililenga kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa wanawake katika uongozi.

Jitihada hizo zimehamasisha wanawake kushiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi ambapo idadi ya Wabunge wanawake waliochaguliwa ni 26 kati ya 264 ambayo ni sawa na asilimia 9, Idadi ya Wabunge wanawake viti maalum ni 113, sawa na asilimia 29 ya idadi ya wabunge wote, jumla ya idadi ya Wabunge wanawake ni 143 kati ya Wabunge wote sawa na asilimia 37.4 mwaka 2023 ukilinganisha na asilimia 16 mwaka 2000. Kwa upande wa Madiwani, Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2020) inaonesha ushiriki wa wanawake katika nafasi za Udiwani kama ifuatavyo, Wanawake Madiwani waliochaguliwa ngazi ya Kata ni 260, Kati ya Madiwani 3,953 sawa na asilimia 7. Wanawake madiwani wa viti maalum ni 1,374 sawa na asilimia 25 ya madiwani wote nchini. Jumla ya Madiwani wanawake ni 1,634 kati ya madiwani 5,587 sawa na asilimia 29, Madiwani wanawake wenyeviti wa Halmashauri 5 kati ya Halmashauri 184 na Meya mmoja tu mwanamke nchini (Taarifa ya Interparliamentary Union- IPU Februari, 2022).

Vilevile, asilimia ya wanawake katika nafasi za Makatibu Tawala wa Mikoa imeongezeka kutoka asilimia 19 mwaka 2005 hadi asilimia 30.8 mwaka 2023, Wakuu wa Wilaya waliongezeka kutoka

asilimia 19 mwaka 2005 hadi asilimia 33.1 mwaka 2023 na Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya kutoka asilimia 14 mwaka 2005 hadi asilimia 28.3 mwaka 2023. Aidha, idadi ya majaji wanawake iliongezeka kutoka asilimia 14 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 38.1 mwaka 2023. Aidha, uwiano wa mahakimu wanawake na wanaume katika ngazi ya mahakama za Wilaya imefikia 50:50.
Changamoto zinazokwamisha jitihada za kufikia lengo ni pamoja na:- kuendelea kuwepo kwa mila na desturi hasi; kutokuungwa mkono kwa wagombea wanawake kutokana na kuwa na mtandao mdogo wa kisiasa; ukatili wa kijinsia kwenye siasa hususan wakati wa uchaguzi; uwezo mdogo wa kiuchumi; mgawanyo usio sawa wa majukumu ya kifamilia kwa wanawake ukilinganisha na wanaume na vikwazo katika umiliki wa rasilimali ambao unakwamisha uwezo wao wa kushiriki kikamilifu katika michakato ya kisiasa.

### 1.2.1.9 Haki za Wanawake

Sera ya Mwaka 2000 ililenga kusimamia ulinzi wa haki za wanawake na wasichana nchini. Katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, Serikali ilitia saini na kuridhia mikataba na itifaki mbalimbali za Kikanda na Kimataifa zinazokuza haki za wanawake na wasichana. Mifumo ya ndani ya ulinzi wa wanawake dhidi ya ubaguzi imetolewa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977; Marekebisho ya kifungu cha 130 cha Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 inayotoa adhabu dhidi ya vitendo vya unyanyasaji wa kingono; kutungwa kwa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sura ya 366 ambayo inahakikisha upatikanaji sawa wa fursa za ajira na mafao ya hifadhi ya jamii hasa mafao ya uzazi na Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 marekebisho ya mwaka 2007 yalijumuisha masuala ya upatikanaji wa ajira na fursa sawa kwa wanawake na wanaume.

Pamoja na kutungwa kwa sheria hizo na utekelezaji wa makubaliano ya Kikanda na Kimataifa, bado zipo changamoto zinazoendelea kuathiri upatikanaji wa haki za wanawake nchini. Sababu za kimazingira kama vile rushwa, ucheleweshaji wa kesi na kunyimwa haki za kiuchumi zimebainika kufifisha jitihada za Serikali na wadau za kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake. Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zenye madhara na vikwazo vya kiuchumi na kijamii katika kufikia huduma za kisheria kutokana na vitendo vya ubaguzi na ukatili dhidi ya wanawake na watoto, hivyo kusababisha ukosefu wa usawa wa kijinsia.

Aidha, Sheria ya Ndoa, Sura ya 29 inakataza mwanandoa kutoa adhabu ya kipigo kwa mwenza wake lakini haitoi adhabu ya ukiukaji. Vilevile, Matumizi ya sheria za Bunge na sheria za kimila huwafanya wanawake na wasichana kuendelea kuwa waathirika wa ubaguzi na ukandamizaji. Serikali kwa kutambua hilo, ilifanya marekebisho ya Kanuni ya Adhabu ili kutoa adhabu kwa watu wote wanaojihusisha na vitendo vya ukatili ikiwemo ukeketaji na kutunga Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sura ya 21 inayowatambua watoa huduma za kisheria wakiwemo wasaidizi wa kisheria kwa lengo la kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo wakiwemo wanawake, wajane na watu wenye ulemavu.

### 1.2.1.10 Hifadhi ya Jamii

Mifuko ya hifadhi ya jamii ya hiyari na isiyo ya hiyari imeundwa ili kutoa huduma za kifedha, kiuchumi na kiafya kwa lengo la kuboresha maisha ya wanufaika. Mifuko hiyo ni pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma -PSSSF; Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii wa Mashirika na

Sekta Binafsi- NSSF; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya- NHIF; Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi – WCF; Mfuko wa Maendeleo ya Jamii –TASAF na Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa – iCHF. Mifuko hiyo isipokuwa PSSSF imetoa fursa kwa sekta zisizo rasmi kujiunga na kunufaika kupitia huduma zinazotolewa. Mfano, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii - TASAF kupitia Mpango wa kunusuru kaya maskini unaohudumia kaya milioni 1.1, zenye jumla ya watu milioni 5.2 wanawake wakiwa ni asilimia 52 katika Halmashauri 159 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Kupitia mfuko huu Serikali inaboresha maisha ya kaya maskini kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeanzishwa ili kuboresha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watumishi wa sekta za umma na binafsi. Hadi kufikia Machi 2019, mfuko ulikuwa umesajili jumla ya wanufaika wapya 4,217,211 sawa na asilimia 8 ya wananchi wote. Katika mwaka 2001, Mfuko wa Afya ya Jamii – CHF ulianzishwa ili kuwahudumia wafanyakazi walio katika sekta isiyo rasmi ambapo mwaka 2019 mfuko huu ulihudumia jumla ya wanufaika 13,029,636 ambao ni asilimia 25 ya watu wote nchini. Aidha, mafanikio mengine ni pamoja na mpango wa huduma ya afya bila malipo kwa wajawazito na watoto walio chini ya umri wa miaka 5 na wazee; kuboresha huduma kwa makundi mbalimbali wakiwemo vijana walio katika rika balehe na wanatoka katika kaya maskini. Pamoja na jitihada mbalimbali za Serikali katika kuboresha huduma za mifuko ya jamii, maeneo mengi nchini bado hayajafikiwa na huduma hii. Mifuko ya hifadhi ya jamii inahudumia asilimia 6 tu ya wafanyakazi wote nchini, ambapo idadi kubwa ya wanawake walio katika sekta isiyo rasmi bado hawajafikiwa na huduma hii (FSPPMP, 2020/21-2029/30). Uhaba wa rasilimali fedha katika familia maskini unakwamisha upatikanaji wa huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ambapo zaidi ya robo ya idadi ya watu nchini Tanzania wanaishi katika umaskini uliokithiri. Vilevile, kukosekana kwa taarifa kwa jamii kuhusu huduma za mifuko ya jamii kunachangia wananchi wengi kutojiunga na mifuko ya jamii mbalimbali ikiwemo Mfuko wa Bima ya Afya – NHIF. Katika kutatua changamoto zilizobainishwa, hatua madhubuti zinatakiwa kuchukuliwa na Serikali pamoja na wadau mbalimbali ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa huduma za mifuko ya jamii kwa kuhamasisha jamii kujiunga na huduma ili kuwafikia na kunufaisha makundi yote ya watu katika jamii, wakiwemo wananchi wanaoishi vijijini na wanawake ambao wengi wao wako katika sekta isiyo rasmi.

### 1.2.1.11 Uzito wa Kazi kwa Wanawake

Sera ya Mwaka 2000 iliweka msisitizo katika: kuhakikisha kuwepo kwa mipango ya kitaifa ya kuwapunguzia wanawake uzito wa kazi; kutoa elimu kwa jamii juu ya teknolojia mbalimbali zinazopatikana nchini; kuwepo kwa utaratibu mzuri wa kupatikana, kusambaza na kutoa mafunzo juu ya utengenezaji, uendeshaji na utunzaji wa teknolojia; teknolojia zibuniwe na kusanifiwa kwa kuzingatia uwezo na maumbile ya watumiaji; kuimarisha huduma za jamii na vituo vya kulea watoto wadogo na huduma za afya; teknolojia sahihi za kurahisisha upatikanaji na hifadhi ya maji na Jamii ihamasihwe katika kushiriki kazi kulingana na uwezo wao ambazo zinafanywa na wanawake tu na matumizi ya nishati rahisi na nafuu.

Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 imeonesha kuwa, Serikali imetekeleza jitihada mbalimbali za kupunguza uzito wa kazi kwa wanawake ambapo matokeo yake ni pamoja na:- Upatikanaji wa umeme katika vijiji vipatavyo 10,312 kati ya 12,268 sawa na asilimia 81 ya vijiji vyote hadi kufikia mwaka 2021, Uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika Sera ya Maji (2002) ambapo

ilikuza ushiriki sawa kati ya wanawake na wanaume katika kufanya maamuzi kuhusu miradi ya usambazaji maji katika ngazi ya kijiji. Kuanzishwa kwa Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini – RUWASA ambayo jukumu lake kuu ni kupanga, kubuni, kujenga na kusimamia huduma za majisafi na usafi wa mazingira vijijini chini ya Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira Na.5 ya mwaka 2019. Hadi Desemba 2019, jumla ya vituo vya kuchotea maji 138,987 vilianzishwa, kati ya hivyo 96,952 ni vituo vya maji vinavyofanya kazi na vinahudumia wakazi wapatao 25,456,436, sawa na asilimia 70.1 pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya maji safi kwa wakazi wa mijini kutoka wastani wa asilimia 73 mwaka 2002 hadi kufikia watani wa asilimia 86.5 mwaka 2022 na kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kutoka wastani wa asilimia 50 mwaka 2002 hadi kufikia wastani wa asilimia 74.5 mwaka 2022 na hivyo kuwapunguzia muda wa kutafuta maji hususan wanawake kwa kuwa ndio wenye jukumu la kutafuta maji.

Jitihada nyingine ni pamoja na ujenzi wa vituo vya afya 352 kote nchini na hivyo kupunguza muda wa wanawake kutafuta huduma za afya mbali na makazi. Vilevile, Serikali imeanzisha vituo 2,833 vya kulelea watoto mchana ili kutoa huduma ya malezi na kuhakikisha ulinzi wa watoto wakati wazazi na walezi wao wakijihusisha na shughuli za kiuchumi.

Hatua nyingine zinazolenga kumpunguzia mzigo wa kazi kwa mwanamke ni pamoja na kuandaliwa kwa Dira na Mkakati wa Serikali unaolenga kuhakikisha ifikapo 2033 asilimia 80 ya watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia ili “Kumtua Mama Kuni Kichwani’’; kutolewa kwa mitungi ya gesi 1,900 kwa wanawake katika mikoa yote 26 inayolenga kuchochea na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia; kutolewa kwa majiko ya gesi 120 na mitungi ya gesi 120 kwa mama lishe ili kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia. Aidha, kufikia 2023 asilimia 76.7 ya vijiji vya Tanzania Bara vimeuganishwa na huduma ya umeme kupitia Programu ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Hatua hii imeongeza uzalishaji na uongezaji wa thamani katika bidhaa zinazozalishwa katika miradi/biashara za wanawake wajasiriamali na hivyo kukuza uchumi wa kaya na pato la Taifa kwa ujumla. Pamoja na jitihada za kukabiliana na mzigo wa kazi kwa wanawake nchini, tatizo bado ni kubwa kulingana na matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika kati ya mwaka 2014 hadi 2022. Kwa mfano, Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2014 unaonesha asilimia 13.6 ya wanawake wanatumia muda mwingi zaidi ukilinganisha na wanaume (asilimia 3.6) katika huduma za nyumbani pekee.

Hivyo, Serikali inapaswa kuendeleza jitihada na kutenga rasilimali za kutosha kuboresha utoaji wa huduma muhimu za kijamii kwa kuzingatia mahitaji na usawa wa kijinsia. Huduma hizo ni pamoja na: usambazaji wa umeme na maji katika maeneo ya vijijini, ujenzi wa vituo vya afya, vitendea kazi vya kilimo kwa kutumia zana na teknolojia za kisasa ambazo zitaongeza tija na kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake sambamba na kumarisha hali zao za lishe. Juhudi za pamoja pia zinahitajika katika kushughulikia mila na desturi hasi zinazoathiri mgawanyo wa majukumu ya kijinsia hususan yale yanayohusu kazi za malezi na matunzo ya familia.

#### 1.2.1.12 Jinsia na Nishati

Uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika Sekta ya Nishati ni nyenzo muhimu katika kutatua athari za pengo la jinsia kwa mwanamke kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kimazingira. Nchini

Tanzania wanawake wanaathirika zaidi na ukosefu wa huduma ya nishati za kisasa na nafuu kutokana na wingi wa majukumu ya kifamilia na malezi, ushiriki mdogo katika masuala ya kijamii na kisiasa. Utafiti wa Hali ya Upatikanaji na Matumizi ya Nishati (2020) ulikusanya taarifa kuhusu huduma ya kuunganishwa kwa umeme kwenye kaya ambapo matokeo ya utafiti huo yalionesha kwamba asilimia 37.7 ya kaya Tanzania Bara zilikuwa zimepata huduma ya umeme katika mwaka 2020. Aidha, utafiti huo ulibaini tofauti za kuunganishwa na huduma ya umeme kati ya kaya za mijini na za vijijini katika mwaka 2016 ilikuwa ni asilimia 73.2 mijini na vijijini asilimia 24.5 tu. Utafiti huo unaonesha kukua na kuimarika kwa huduma ya umeme nchini ambayo inaongeza ushiriki wa wanawake na wanaume katika shughuli za kiuchumi, kuboresha utoaji wa huduma za kijamii kama vile afya na elimu, na hivyo kuimarisha maisha ya watu vijijini na mijini.

Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa umeme kwa bei nafuu, kutumia huduma za kisasa na kwa ufanisi. Mikakati hii ni pamoja na: Kufanya mapitio ya Sera ya Nishati ya mwaka 2003 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2015; Kutunga Sheria ya Nishati Vijijini ya mwaka 2005; na Sheria ya Umeme Na.10 (2008) ambayo ilifuta Sheria ya Umeme Sura ya 131 . E. 2002]. Serikali pia imeanzisha mifumo bora ya bei nafuu na yenye kuaminika inayorahisisha upatikanaji wa nishati ya umeme. Mifumo hiyo ni pamoja na kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji - EWURA na Bodi ya Nishati Vijijini – REB iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Nishati Vijijini, (2005); Wakala wa Nishati Vijijini – REA na Mfuko wa Nishati Vijijini -REF ulioanzishwa kupitia Sheria ya Bunge Na.8 ya mwaka 2005 ili kukuza na kuwezesha upatikanaji wa huduma za nishati ya kisasa katika maeneo ya vijijini.

Mafanikio mengine yaliyobainishwa kwenye Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 ni pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya gesi (LPG) ya kupikia nchini kufikia tani 244,732; wananchi hususan wa vijijini kuendelea kupata uelewa kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ikiwa ni pamoja na kupunguza uwezekano wa kupata magonjwa katika mfumo wa kupumua na vifo hususan kwa wanawake. Pamoja na juhudi na maendeleo yaliyofikiwa ikiwa ni huduma za kisasa za bei nafuu na zinazoaminika za nishati (umeme), nishati safi ya kupikia bado haitoshi. Huduma za kijamii katika baadhi ya vijiji nchini ikihusisha vituo vya afya na zahanati hazijapata huduma ya umeme na hivyo kuathiri utoaji wa huduma za afya hususan kwa wanawake wakati wa kujifungua. Aidha, changamoto katika utoaji wa huduma ya umeme zinatishia ukuaji na maendeleo ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ambazo hutegemea upatikanaji wa umeme ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za mawasiliano na uendeshasji wa biashara ndogo na za kati. Changamoto nyingine ni uharibifu mkubwa wa mazingira unaosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa kama chanzo kikuu cha nishati ya kupikia. Hivyo, ni muhimu kwa mipango ya usambazaji na matumizi ya nishati kuzingatia mahitaji ya wanawake, wanaume, wavulana na wasichana ili kuhakikisha huduma ya kisasa ya nishati inawanufaisha watu wote kwa usawa.

### 1.2.1.13 Wanawake, Amani na Usalama

Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama (Women, Peace and Security-WPS) ni utekelezaji waAzimio Na. 1325 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2000) ambalo lilitambua athari hasi kwa wanawake kutokana na migogoro katika jamii ikiwa ni pamoja na kutambua jukumu muhimu walilonalo katika kuzuia migogoro na kujenga amani. Vilevile, ajenda hii inakuza dhana ya amani na

usalama ili kujumuisha masuala ya kijinsia katika ulinzi na usalama wa binadamu, kuzuia vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wanawake na wasichana, kutoa msaada wakati wa migogoro/majanga na urejeshaji wa amani kwenye jamii (relief and recovery). Bara la Afrika limezingatia ajenda hii kupitia mnyororo wa matokeo (Continental Result Framework) wa mwaka 2018 kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa Ajenda ya Amani na Usalama kwa Wanawake. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja ya nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu zinazotekeleza Azimio Na. 1325 kupitia Mpango Mkakati wa Kikanda (2018 - 2023), Mkakati wa Kikanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika kuhusu Wanawake, Amani na Usalama (2018 - 2022) na Mkakati wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (2015 - 2019).

Tanzania inatambulika Kimataifa kuwa miongoni mwa nchi zenye amani zaidi Duniani, ambapo imeorodheshwa kuwa ni nchi ya 58 kati ya nchi 163 kwa mujibu wa Fahirisi ya Amani ya Dunia ya 2021. Vilevile, ilishika nafasi ya 76 kati ya nchi 170 kwenye Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama kwa sawa na ongezeko la asilimia 10 ikilinganishwa na takwimu za Mwaka 2017. Aidha, Tanzania ni nchi ya mfano katika kuhifadhi wakimbizi kutoka nchi jirani tangu mwaka 1970, ambapo hadi Desemba 2022, ilipokea wakimbizi na wanaotafuta hifadhi jumla 247,207 wengi wao ni wanawake na watoto. Tanzania pia imechangia walinda amani 1,482 wakiwemo wanawake 124 katika Operesheni tofautiza Ulinzi wa Amani za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika hivyo kuifanya Tanzania kuwa nchi ya13 ya wachangiaji wakuu duniani na ya 6 kwa nchi za Afrika.

Pamoja na jitihada hizo, changamoto zilizopo ni uelewa mdogo kuhusu Amani na Usalama kwa Wanawake hususan katika masuala ya ulinzi na usalama, uokoaji wakati wa majanga, mikakati ya kuzuia migogoro na majanga na kujenga upya jamii baada ya majanga na migogoro; Uwakilishi mdogo wa wanawake katika mifumo ya amani na usalama ikiwemo Kamati za Ulinzi na Usalama katika ngazi mbalimbali za jamii; Miundo rasmi na isiyo rasmi ya usuluhishi wa migogoro ikiwemo mbinu za asili za usuluhishi wa migogoro; Ushiriki mdogo wa wanawake katika usuluhishi wa migogoro na operesheni za walinda amani; na Uwepo wa vitendo vya udhalilishaji, unyanyasaji wa kingono na kijinsia panapotokea majanga na migogoro katika jamii.

Katika kukabiliana na changamoto zilizobainishwa, mbinu za zinazotumika kuzuia migogoro ni muhimu zizingatie masuala ya kijinsia. Aidha, katika maeneo ambayo mifumo hiyo bado haijaanzishwa, ni muhimu ianzishwe kwa kuzingatia usawa wa jinsia.

### 1.2.1.14 Haki na Usawa Kiuchumi

Tanzania inatekeleza malengo ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (Generation Equality Forum – GEF) ambalo linajumuisha mkakati wa Kimataifa wa kuongeza kasi ya kutekeleza afua za kuelekea kwenye usawa wa kijinsia Duniani. Jukwaa hili linatokana na maadhimisho ya miaka 25 ya Azimio la Ulingo wa Beijing ambapo Jumuiya ya Kimataifa ilitambua hatua za maendeleo ya utekelezaji wa afua zilizofikiwa duniani kote kuelekea usawa wa kijinsia. Hata hivyo, Ripoti Endelevu ya Umoja wa Mataifa (2020) na Tamko la Kisiasa la Umoja wa Mataifa lililopitishwa tarehe 09 Machi, 2020 wakati wa kikao cha 64 cha Kamisheni ya Umoja wa Mataifa kuhusu Hali ya Wanawake Duniani, ilibainika kuwa hakukuwa na nchi ambayo imetekeleza kikamilifu ahadi za Azimio la Ulingo wa Beijing.

Tanzania iliweka ahadi katika Jukwaa hilo za kutekeleza eneo la Haki na Usawa Kiuchumi ili kuongeza kasi ya kufikia usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake na kunufaika na ukuaji wa Uchumi. Ahadi hizo zinatokana na kutambua kuwa jitihada za kufikia usawa wa kijinsia hudhoofishwa na maendeleo yaliyopatikana hurudishwa nyuma kutokana na kuwepo kwa tamaduni zenye madhara dhidi ya wanawake na wasichana, ushiriki usio na usawa, mipango na bajeti isiyozingatia usawa wa kijinsia. Aidha, kuwepo kwa sheria zinazochangia kukosekana kwa usawa wa kijinsia na mzigo mkubwa wa kazi za nyumbani kwa wanawake na wasichana pamoja na madhara ya Janga la UVIKO-19 vimechangia pia kudhoofisha kasi ya maendeleo.

### 1.2.1.15 Ukatili wa kijinsia

Tanzania kama nchi nyingine duniani ina idadi kubwa ya watoto wa kike na wa kiume, wanawake na wanaume ambao wamekuwa wakifanyiwa ukatili wa aina mbalimbali kama vile ukatili wa kingono, kimwili, kiuchumi na kisaikolojia. Kwa mujibu wa Takwimu za hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani kwa mwezi Januari hadi Mei, 2022 Matukio ya vitendo vya ukatili wa kijinsia yanayoongoza ni pamoja na ubakaji, unajisi, kuzini na maharimu, shambulio la aibu, na utekaji. Aidha, kati ya hayo vitendo vya ubakaji vimeshika nafasi ya kwanza kwa idadi ya matukio (2,445) ikifuatiwa na kulawiti (555). Hii ina maana kuwa jitihada kubwa zinahitajika katika kupambana na matukio haya ya ukatili ambao unaleta athari kubwa katika maendeleo na ustawi wa watoto wa kike na wa kiume.

Matokeo ya utafiti wa SIGI (2022) yanaonesha kuwa asilimia 55 ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 wameshawahi kufanyiwa aina mojawapo ya ukatili, ambapo asilimia 16 walifanyiwa ukatili wa kisaikolojia, asilimia 15 ukatili wa kimwili, asilimia 9 ukatili wa kiuchumi na asilimia 7 ukatili wa kingono. Hata hivyo, ukatili wa kimwili umepungua hadi kufikia 15 (SIGI, 2022) ikilinganishwa na 40 (TDHS/MIS, 2015/16).

Katika kupambana na vitendo vya ukatili, Serikali imeendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kutoa taarifa kwenye vyombo husika na kuimarisha huduma kwa manusura wa vitendo vya ukatili. Aidha, bado msukumo wa kisera unahitajika ili kutokomeza hali hii ya ukatili wa kijinsia nchini.

### 1.2.1.16 Jinsia na Takwimu

Upatikanaji wa takwimu za kijinsia ni muhimu katika kupanga, kufanya maamuzi na utoaji wa taarifa. Tathmini ya utekelezaji wa Sera imebaini kuwepo kwa umuhimu wa kujenga uelewa wa uandaaji wa mipango yenye mtazamo wa kijinsia. Aidha, uwepo wa takwimu zilizochanganuliwa kijinsia zitasaidia uamuzi sahihi katika kuandaa mipango na afua zenye mtazamo wa kijinsia katika sekta zote.

Baadhi ya Wizara za kisekta kama Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wizara ya Afya zimefanya jitihada katika kukusanya, kuchakata na kutumia takwimu za kijinsia. Hata hivyo, bado kumekuwa na mwitikio mdogo katika Wizara za Kisekta kuhusu kuchanganua takwimu kwa mrengo wa kijinsia. Hivyo, ipo haja ya kuhamasisha na kuwajengea uwezo wa masuala ya takwimu zenye mrengo wa kijinsia.

### 1.2.1.14 Jinsia na Utawala Bora

Utawala bora unajumuisha kuheshimu utawala wa sheria, demokrasia, ushiriki katika kufanya maamuzi, uwazi na uwajibikaji, pamoja na kulinda haki za binadamu. Katika muktadha huu, usawa wa kijinsia ni muhimu katika kuzingatia misingi ya utawala bora kwani unahakikisha ushiriki mzuri wa wanawake na wanaume katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimazingira.
Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ambayo inalenga kukuza usawa wa kijinsia nchini. Mipango hii ni pamoja na k uanzishwa k wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB); Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na Mkakati wa Kuongeza idadi ya wanawake katika nafasi za uongozi kama vile Bunge na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, Serikali bado haijafikia lengo la usawa wa kijinsia la Umoja wa Afrika (AU) la hamsini kwa hamsini (50/50).

Pamoja na kwamba taarifa ya tathmini imeonesha jitihada zinazoendelea kutekelezwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya kijinsia nchini, bado upo umuhimu wa kuweka mwelekeo wa kisera kuhusu uzingatiaji wa masuala ya jinsia na maendeleo ya wanawake katika utawala bora.

## 1.2.2 Mafanikio

Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000 ilionesha mafanikio katika kukuza usawa wa kijinsia nchini. Mafanikio hayo ni pamoja na: -

i) Uzingatiaji wa masuala ya Kijinsia kwenye mifumo mbalimbali katika Sera za kisekta, Sheria na Programu zikiwemo Sera ya Maji (2002); Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (2003); Sera ya Afya (2007); Sera ya Taifa ya Kilimo (2013); Sera ya Elimu na Mafunzo (2014); Sera ya Taifa ya Huduma ndogo za Fedha (2017); Sera ya Taifa ya Mazingira (2021); Sheria ya Majisafi na Usafi wa Mazingira, Sura ya 272; Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410; Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa, Sura ya 290; Mipango Mikakati ya Maendeleo ya Kitaifa na Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 - 2021/22); na Mkakati wa Nne wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Tanzania (2018/19- 2022/23). Aidha, kuandaliwa kwa nyaraka mbalimbali za kushugulikia masuala ya kijinsia katika Taasisi ikiwemo Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati na maeneo ya umma;

ii) Kuongezeka kwa ushiriki wa wanawake katika nafasi mbalimbali za uongozi na maamuzi. Mfano, Kwa mara ya kwanza Tanzania imepata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu; Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu mbili. Vilevile, idadi ya Mawaziri wanawake imeongezeka kutoka asilimia 21 mwaka 2015 hadi asilimia 37.4 mwaka 2023, idadi ya Makatibu wakuu Wanawake imeongezeka kutoka asilimia 13.8 mwaka 2015 mpaka kufikia asilimia 22.2 mwaka 2023 na idadi ya Wakurugenzi wa Halmashauri Wanawake imeongezeka kutoka asilimia 16.4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 28.3 mwaka 2023;

iii) Utoaji wa mikopo katika Halmashauri mbalimbali kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya mikopo isiyo na riba kwa mgawanyo wa wanawake asilimia 4, vijana asilimia 4 na watu wenye ulemavu asilimia 2 imewezesha kuanzishwa na kukua kwa miradi yenye matokeo chanya. Baadhi ya vikundi vilivyonufaika ni MIOMBO Beekepers Initiatives Group cha Tabora kilichoanzisha kiwanda cha kuchakata mazao ya

asali; Kikundi cha Wanawake cha Juhudi cha Jijini Dar es salaam chenye kumiliki kiwanda cha kutengeneza sabuni na dawa za usafi; Kiwanda cha Hand Product of Tanzania cha kutengeneza Batiki; na Kikundi cha NURU Disabled kinachojishughulisha na usafirishaji wa mizigo ambacho kinamiliki Lori aina ya SCANIA na kikundi cha Bulldozer Youth Group cha Jijini Tanga cha uvuvi na uuzaji wa samaki kinachomiliki boti ya uvuvi.

iv) Kupungua kwa vifo vitokanavyo na uzazi nchini kutoka vifo 578 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2004/05 hadi kufikia vifo 432 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2019. Hali hii imesababishwa na kuongezeka kwa uelewa juu ya umuhimu wa afya ya uzazi miongoni mwa jamii na uzingatiaji wa huduma rafiki kwa wanawake kwenye vituo vya afya pamoja na kuwepo kwa programu mbalimbali za afya zenye mtazamo wa kijinsia.

v) Kuongezeka kwa udahili wa wasichana kwa darasa la I – VII kutoka 8,298,377 (wasichana 4,218,377 na wavulana 4,079,905) mwaka 2015 hadi kufikia 11,196,788 (wasichana 5,639,081 na wavulana 5,557,707) mwaka 2021. Katika elimu ya Sekondari, idadi ya wanafunzi walioandikishwa kidato cha 1 - 6 iliongezeka kutoka wanafunzi 1,774,383 (wasichana 953,394 na wavulana 871,410) mwaka 2015 hadi wanafunzi 2,671,927 (wasichana 1,389,613 na wavulana 1,282,314) mwaka 2021 (BEST, 2021); na

vi) Kuongezeka kwa upatikanaji na umiliki wa ardhi kwa wanawake ambapo hadi kufikia 2021/22 jumla ya Hatimiliki za Kimila 1,171,884 zimetolewa kwa wanawake 406,915 na Wanaume 764,969. Aidha, Hatimiliki 916,765 zilitolewa kwa wanawake 228,203 na wanaume 688,562.

### 1.2.3 Upungufu

Katika uandaaji wa Sera ya Mwaka 2000 kuna baadhi ya masuala ya kijinsia ambayo hayakujumuishwa katika Sera hiyo na hivyo kukosa matamko ya kisera. Miongoni mwa masuala hayo ni: kutojumuisha aina nyingine za ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili wa kisaikolojia, ukatili mitandaoni, ukatili wa kimwili na kingono; masuala ya jinsia na afya hususan uhimizaji wa wanawake, wasichana, wanaume na wavulana kuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ikiwemo magonjwa ya saratani ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume; masuala ya Amani na Usalama kwa Wanawake wakati wa migogoro na majanga pamoja na ushiriki wao kwenye programu za ulinzi na amani; kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi kwa kuanzisha na kuendeleza vituo vya jamii vya malezi na makuzi ya awali ya Watoto ili kushiriki katika shughuli za uzalishaji; Jinsia na Huduma za Kidijitali. Vilevile, Sera ya Mwaka 2000 haikushughulikia masuala mtambuka ikiwemo utawala bora na UKIMWI hivyo kukosa matamko ya kisera.

### 1.2.4 Changamoto

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, zipo changamoto zilizoathiri kufikiwa kwa malengo ya Sera. Changamoto hizo ni pamoja na: -

i) Kuendelea kuwepo kwa umaskini wa kipato kwa wanawake hususan wanaoishi vijijini, waofanya kazi kwenye sekta isiyo rasmi na wenye ulemavu;

ii) Kuendelea kuwepo kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili wa mtandaoni, kimwili, kingono, kisaikolojia na kiuchumi;

iii) Uwiano usio sawa katika nafasi za uongozi na maamuzi baina ya wanawake na wanaume katika ngazi mbalimbali;

iv) Kuendelea kuwepo kwa vifo vya mama wajawazito, ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa ikiwemo saratani, tezi dume na afya ya akili kwa wanawake na wanaume pamoja na ugumu wa kufikia huduma za afya hususan kwa wanawake waishio vijijini.

v) Fikra hasi kuhusu ushiriki wa wasichana kwenye masomo ya STEM, umaskini wa kipato, mgawanyo wa majukumu usio sawa kati ya watoto wa kike na wa kiume, ndoa na mimba za utotoni, upungufu wa miundombinu inayozingatia mahitaji ya kijinsia shuleni pamoja na mila na desturi hasi zenye kumnyima mtoto wa kike fursa ya elimu;

vi) Kutokuzingatia usawa wa kijinsia kwenye shughuli za kiuchumi unaotokana na uwepo wa mipango na bajeti isiyo na mrengo wa kijinsia, uwiano usio sawa wa majukumu katika umiliki wa rasilimali za uzalishaji pamoja na ushiriki na ufikiaji mdogo wa huduma jumuishi za kifedha na kwenye kazi zenye staha;

vii) Ushiriki mdogo wa wanawake kwenye ubunifu na utumiaji wa teknolojia za kidijitali na zisizo za kidijitali katika shughuli za uzalishaji mali na mnyororo wa thamani;

viii) Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zinazowanyima wanawake fursa ya kumiliki na kutumia rasilimali;

ix) Upatikanaji na utumiaji hafifu wa takwimu zilizochanganuliwa kijinsia katika kupanga, kutekeleza na kutathmini mipango ya maendeleo katika sekta zote;

x) Ushiriki mdogo wa wanaume katika kukuza usawa wa kijinsia;

xi) Ufikiaji hafifu wa wanawake kwenye mifumo ya Haki na Sheria kutokana na vikwazo vya kijamii na kiuchumi;

xii) Uelewa mdogo wa ajenda ya amani na usalama kwa wanawake ikiwemo ushiriki hafifu wa wanawake katika mifumo ya amani na usalama Kitaifa na Kimataifa;

xiii) Kuendelea kuwepo kwa maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI miongoni mwa wasichana, wanawake, wavulana na wanaume; na

xiv) Madhara yatokanayo na mabadiliko ya tabianchi na athari za uharibifu wa mazingira kwa wanawake pamoja na ushiriki mdogo katika usimamizi na utunzaji wa mazingira.

Kutokana na kuwepo kwa changamoto na upungufu uliobainishwa, Sera hii imejumuisha maeneo ya kisera yanayotoa mikakati ya kutatua changamoto na upungufu huo. Aidha, Sera hii imezingatia na kujumuisha afua na maudhui yaliyomo katika Mipango, Dira, Mikataba, Maazimio, Itifaki, Sera na Sheria mbalimbali katika ngazi ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa ambazo zimetungwa, zimeridhiwa na zinazotekelezwa nchini.

# SURA YA PILI
# UMUHIMU WA SERA, DIRA, DHIMA NA MALENGO

## 2.1 Umuhimu wa Sera

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama nchi iliyoridhia na kutia saini Mikataba ya Kikanda na Kimataifa, Itifaki na Matamko yanayohimiza kuwepo kwa usawa wa kijinsia, inawajibika kutunga sera zinazohimiza usawa wa kijinsia. Takwimu na Mapitio ya maandiko mbalimbali yanaonesha kwamba, idadi kubwa ya changamoto, upungufu na masuala mapya yaliyojitokeza yalikuwa kikwazokatika kufikia usawa wa kijinsia kupitia utekelezaji wa mikakati iliyobainishwa na Sera ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2000 na Mkakati wa Utekelezaji wake wa mwaka 2005.

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 inalenga kutatua changamoto na upungufu wa kisera unaojumuisha: Kuendelea kuwepo kwa mila na desturi zinazowanyima wanawake fursa ya kumiliki na kutumia rasilimali; Kukosekana kwa matamko ya kisera yenye lengo la kushughulikia vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vimeendelea kuwepo; Changamoto ya upatikanaji wa takwimu zenye mtazamo wa kijinsia ili kuleta uwiano ulio sawa katika shughuli za mipango ya maendeleo; Kuwepo kwa uelewa mdogo wa dhana ya usawa wa kijinsia miongoni mwa jamii; Ajenda ya Wanawake, Amani na Usalama; Jinsia na Huduma za Kidijitali; Jinsia na Utawala Bora na Ushiriki mdogo wa wanaume katika kukuza usawa wa kijinsia.

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 inalenga kujumuisha masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Sera ya Mwaka 2000. Masuala hayo ni pamoja na kuongeza ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za uongozi na maamuzi kutoka uwiano wa 30:70 ya lengo la mwaka 2005 hadi kufikia 50:50 ya wanawake na wanaume kama ilivyobainishwa katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), Agenda ya Afrika Tuitakayo, 2063, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 – 2026/27. Pamoja na hayo, Sera inahamasisha kujumuisha masuala ya kifedha kwa wanawake katika sekta isiyo rasmi na sekta binafsi; kuhimiza matumizi ya teknonojia ya uchumi wa kidijitali kwa wanawake; kuhamasishwa mabadiliko ya mifumo ya kisheria ili kukuza usawa wa kijinsia katika umiliki na urithi wa mali; na kutoa miongozo kuhusu uanzishwaji na uendelezaji wa Jukwaa la uwezeshaji wanawake Kiuchumi.

## 2.2 Dira, Dhima na Malengo ya Sera

### 2.2.1 Dira

Jamii yenye haki na usawa wa kijinsia ambapo wanawake na wanaume wanaishi kwa pamoja na kufaidika kwa usawa kutokana na fursa zilizopo za kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi.

### 2.2.2 Dhima

Kukuza usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha na maendeleo ikiwa ni pamoja na nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kupitia maendeleo na utekelezaji wa sera, mikakati, programu, miradi na mipango inayozingatia na kulinda ustawi wa wanawake na wanaume; wavulana na wasichana na kuimarisha ukuaji na maendeleo ya uchumi wa Taifa.

### 2.2.3 Lengo la Sera

Lengo kuu la Sera hii ni kukuza haki na usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha na maendeleo.

### 2.2.4 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kukuza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa fursa za kiuchumi na mitaji kwa wanawake na wanaume;

(ii) Kutokomeza aina zote za ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili wa kijinsia mitandaoni;

(iii) Kuwa na jamii inayoheshimu usawa na haki kwa wote;

(iv) Kuimarisha ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za uongozi na maamuzi;

(v) Kukuza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa elimu bora na mafunzo;

(vi) Kuboresha huduma za afya jumuishi zikiwemo afya ya uzazi na magonjwa yasiyoambukizwa kwa wanawake na wanaume;

(vii) Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika uwezeshaji wa wanawake;

(viii) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa takwimu za kijinsia;

(ix) Kuzingatia masuala ya kijinsia katika mifumo na programu za wanawake amani na salama;

(x) Kuhamasisha misingi ya utawala bora inayozingatia masuala ya kijinsia.;

(xi) Kuhimiza uzingatiaji wa huduma na kujikinga na maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI kwa wanaume na wanawake; na

(xii) Kukuza uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika usimamizi wa mazingira.

# SURA YA TATU
# MASUALA YA KISERA, MALENGO NA MATAMKO

## 3.1 Utangulizi

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake imeweka mfumo wa Kitaifa wa uratibu wa masuala ya kukuza usawa wa kijinsia nchini. Sera hii inatambua wajibu wa sera za kisekta katika uzingatiaji wa usawa wa kijinsia kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi. Kwa kuzingatia hilo, mafanikio yanayotarajiwa wakati wa utekelezaji wa sera hii yanategemea ujumuishwaji wa masuala ya kijinsia katika sera za kisekta. Hivyo basi, sura hii inaelezea Masuala ya Kisera, Malengo na Matamko yanayohusu changamoto za kijinsia nchini.

## 3.2 Masuala ya Kisera

### 3.2.1 Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi

**Maelezo:**

Maendeleo ya Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake Kiuchumi ni fursa muhimu katika kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa kuhakikisha ushirikishwaji wa wanawake katika kumiliki na kutumia rasilimali za uzalishaji. Kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa (2021) inaonesha kuwa shughuli nyingi za kiuchumi hususan katika sekta ya kilimo, misitu na uvuvi hufanywa na wanawake, ambapo kati ya watu 15,448,091, wanawake 7,686,198 wanajishughulisha na kazi hizo za kilimo, misitu na uvuvi. Hata hivyo, pamoja na kuwa wanawake ni wengi kwa zaidi ya asilimia 51 (Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi, 2022) mgawanyo wa fursa za kiuchumi kati ya wanawake na wanaume hauko sawa katika sekta mbalimbali ikiwemo madini ambapo takwimu kutoka katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa (2021), hali ya ajira kwa sekta ya madini imeonesha kuwa ni wanawake 41,538 kati ya watumishi 218,353 sawa na asilimia 19 ya ajira katika sekta hiyo ikifuatiwa na sekta ya ujenzi yenye idadi ndogo ya wanawake walioajiriwa ambayo ni wanawake 18,607 kati ya watumishi 568,774 sawa na asilimia 3.2.

Pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, malengo ya uwezeshaji wanawake kiuchumi hayajafikiwa kikamilifu kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo huduma za kibenki kutofika katika maeneo mengi ya vijijini; ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo unaochangiwa na matumizi ya mbinu duni za uzalishaji; ukuaji mdogo wa masoko ya kilimo na kukosekana kwa mnyororo wa thamani wenye tija; miundombinu duni katika maeneo ya vijijini hususan barabara, mawasiliano ya simu na nishati. Aidha, kukosekana kwa dhamana (collateral) kumebainika kusababisha wanawake kukosa mitaji kutokana na kushindwa kufikia vigezo vya kukopesheka katika taasisi za fedha ambapo katika Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa (2020) inaonesha wanufaika wa mikopo ya nyumba iliyotolewa na benki na taasisi za fedha walikuwa 1,345 ambapo wanaume walikuwa 889, wanawake 389 na waliokopa kwa pamoja walikuwa 67. Vilevile, wanawake walio katika sekta zisizo rasmi mijini na vijijini hawajafikiwa na huduma za hifadhi ya jamii kutokana na hali duni ya kiuchumi.

Pamoja na kuwepo kwa mila na desturi chanya ambazo zinapaswa kuendelezwa katika jamii, bado kuna mila na desturi kandamizi zinazowafanya wanawake kushindwa kunufaika na shughuli zao za kiuchumi. Baadhi ya mila na desturi hizo ni kama vile utunzaji wa misitu na vyanzo vya maji ambayo jamii iliaminishwa kuwa miungu yao inaishi hapo na dhana iliyojengeka katika malezi kuwa mtoto ni wa wote na kila mwanajamii anajukumu la kumlea. Mila na desturi hasi ni pamoja na kuzidi kuongezaka kwa umaskini na utegemezi unatokana na mfumo dume hasa kwenye masuala ya haki ya kumiliki mali.

Aidha, wanawake wengi wanakabiliwa na umaskini wa muda kutokana mzigo wa kazi za nyumbani hivyo kukosa muda wa kushiriki katika shughuli za kiuchumi. Hivyo, ni muhimu kuweka mikakati madhubuti na jumuishi yenye kutoa matokeo chanya katika jitihada za kuwawezesha wanawake kiuchumi.

### Lengo la Kisera

Kukuza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa fursa za kiuchumi na kifedha kwa wanawake na wanaume.

### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji itakayowezesha wanawake kufanya shughuli za uzalishaji mali;

(ii) Kuimarisha ushiriki wa wanaume na wanawake katika kutambua na kutumia fursa zitakazowawezesha kujikwamua kiuchumi;

(iii) Kujenga uelewa kwa wanaume kuhusu umuhimu wa kushiriki katika kazi za nyumbani ikiwemo huduma za malezi;

(iv) Kukuza ushiriki wa jamii katika kuendeleza mila na desturi chanya na kuondokana na mila na desturi zenye madhara kwa makundi mbalimbali kama vile wanawake, wajane na wagumba; na

(v) Kuimarisha mifumo jumuishi ya hifadhi ya jamii kwa sekta rasmi na zisizo rasmi mijini na vijijini.

## 3.2.2 Ukatili wa Kijinsia

### Maelezo:

Serikali kwa kushirikiana na wadau imetekeleza jitihada mbalimbali za kutokomeza ukatili wa kijinsia katika jamii. Jitihada hizi zimesaidia kuongezeka kwa utoaji wa taarifa kuhusu vitendo vya ukatili sambamba na kuimarika kwa utoaji wa huduma kwa manusura wa ukatili. Mwaka 2021, Serikali iliendelea kufuatilia na kudhibiti makosa ya ukatili na unyanyasaji wa kijinsia ikiwemo ubakaji, ulawiti, kutupa watoto, wizi wa watoto, ukeketaji na vipigo kupitia Dawati la Polisi la Jinsia na Watoto. Takwimu zinaonesha kuwa vitendo vya ukatili vimepungua kutoka matukio 41,416 (Me 13,471 na Ke 27,945) mwaka 2017/18 hadi kufikia 29,373 (me 8,476 na ke 20,897) mwaka 2020/21. Kupungua kwa matukio haya kumetokana na jitihada mbalimbali za Serikali na wadau. Hata hivyo, tatizo la ukatili dhidi ya wanawake limeendelea kushamiri ikiwemo ukatili wa kijinsia mtandaoni unaotokana na mmomonyoko wa maadili na malezi duni.

Kuendelea kuwepo kwa vitendo hivi katika jamii kunasababisha maumivu kwa wanawake na watoto, kuathiri ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi na kijamii na hivyo kupunguza uwezo wao wa kujikwamua dhidi ya umaskini. Taarifa ya Utafiti wa Masuala ya Jinsia, Mila, Desturi, Tamaduni na Sheria za Tanzania (SIGI, 2022) inaonesha kuwa asilimia 38 ya wanawake wenye umri wa miaka 15 – 49 wamefanyiwa ukatili. Masuala yanayosababisha kuongezeka kwa ukatili ni pamoja na; hofu ya kutengwa na jamii baada ya kutoa taarifa za ukatili, ucheleweshaji wa kesi za ukatili wa kijinsia mahakamani, uwepo wa mifumo dume katika jamii na upatikanaji duni wa huduma za kijamii na afya kwa manusura wa ukatili.

### Lengo la Kisera

Kutokomeza aina zote za ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili wa kijinsia mitandaoni.

### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kukuza uelewa kuhusu athari za ukatili wa kijinsia ikiwemo ukatili mtandaoni unaotokana na matumizi yasiyo sahihi ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano;

(ii) Kuimarisha mifumo ya kuzuia na kudhibiti ukatili wa kijinsia;

(iii) Kuunda, kuimarisha na kuendeleza mifumo ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia katika jamii;

(iv) Kuhamasisha na kuendeleza malezi na makuzi chanya yanayozingatia jinsia katika ngazi ya familia na jamii katika kukabiliana na mmonyoko wa maadili; na

(v) Kuimarisha ushirikishwaji wa wanaume, viongozi wa dini, kimila, watu mashuhuri na wadau wengine katika jitihada za kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

## 3.2.3 Haki na Usawa Kiuchumi

### Maelezo:

Mabadiliko ya jamii za Kitanzania yanayolenga kuwa na jamii inayoheshimu haki na usawa wa kijinsia ambapo wanawake na wanaume, wasichana na wavulana, wananufaika kwa usawa na fursa zilizopo za kijamii na kiuchumi, yanahitaji msukumo wa kisera na mabadiliko ya fikra na kiutamaduni katika ngazi zote. Aidha, viongozi na jamii wanapaswa kuwa na mtazamo unaokubali kukuza na kuendeleza jitihada za kuleta mageuzi katika kukuza usawa wa kijinsia na kuwezesha kuwepo kwa maadili chanya yanayolenga kuimarisha ulinzi na ustawi wa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana wa vizazi vyote katika nyanja zote za maisha. Kuimarika kwa haki na usawa wa kiuchumi ni nyenzo muhimu katika kukuza uchumi na kuchochea maendeleo ya Taifa. Changamoto za kupatikana kwa haki na usawa kiuchumi ni pamoja na kuwepo kwa mgawanyo usio sawa wa kazi katika ngazi ya familia na jamii ambapo wanawake wanabeba uzito mkubwa wa kazi za nyumbani ikilinganishwa na kiwango cha ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi; kunyimwa haki ya kumiliki rasilimali za uzalishaji, ushiriki na ufikiaji mdogo katika huduma jumuishi za kifedha; na ushiriki mdogo kwenye kazi zenye staha na ujira.

### Lengo la Kisera

Kuwa na jamii inayoheshimu usawa na haki kwa wote.

### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kuimarisha uwekezaji wenye lengo la kupunguza mzigo wa kazi kwa wanawake na wasichana zikiwemo upatikanaji wa huduma za maji, nishati, vituo vya malezi na makuzi ya mtoto;

(ii) Kukuza ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika kazi zenye staha katika sekta rasmi na zisizo rasmi;

(iii) Kuboresha mifumo na utekelezaji ili kukuza upatikanaji na umiliki wa rasilimali za uzalishaji kwa wanawake;

(iv) Kuwekeza kwenye tafiti kuhusu haki na usawa wa kiuchumi kwa wanawake na wanaume; na

(v) Kukuza uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika mipango jumuishi ya uchumi na fedha.

## 3.2.4 Jinsia, Uongozi na Maamuzi

**Maelezo:**

Ushiriki wenye tija wa wanawake na wanaume katika masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ni nyenzo muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia nchini. Vilevile, Serikali imefanya jitihada za makusudi katika kuleta uwakilishi sawa wa wanawake katika mamlaka zinazofanya maamuzi mbalimbali ikiwemo uwepo wa viti maalum. Hata hivyo, zipo changamoto zinazozuia wanawake kushika nafasi za maamuzi zikiwemo mila, desturi na tamaduni kandamizi zinazowanyima wanawake haki ya kushiriki katika uongozi, mgawanyo usio sawa wa majukumu kati ya mwanaume na mwanamke katika kaya, dini, mfumo dume, mitazamo hasi, sheria kandamizi, rushwa, dharau na ukatili na vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake kwenye majukwaa ya kisiasa na hata katika ngazi ya familia na jamii kwa ujumla. Pamoja na uwepo wa miongozo na matamko mbalimbali, bado upo umuhimu wa kuongezajitihada za kumpa mwanamke fursa ya kushiriki au kushirikishwa kikamilifu katika ngazi za maamuzi.

### Lengo la Kisera

Kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake ili kushiriki kikamilifu katika ngazi zote za uongozi na maamuzi.

### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kukuza usawa na ushiriki jumuishi wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana katika ngazi zote za uongozi na maamuzi; na

(ii) Kukuza uelewa kwa jamii kuhusu haki ya wanawake kushiriki katika ngazi zote za uongozi na maamuzi.

### 3.2.5 Jinsia, Elimu na Mafunzo

#### Maelezo:

Sera imechangia katika kuongeza ushiriki wa watoto wa kike kwenye elimu ikiwemo ongezeko la udahili, uhitimu, mapitio ya mitaala, ujenzi wa miundombinu rafiki inayowezesha wasichana kushiriki kikamilifu darasani, mabadiliko ya mifumo ya kisheria na ufadhili maalum kwa wasichana ili waweze kujiendeleza katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hesabu. Pamoja na jitihada hizo, ushiriki wa wasichana katika elimu ya juu hususan kwenye masomo ya STEM umeendelea kuwa mdogo kutokana na fikra hasi kuhusu ushiriki wa wasichana kwenye masomo ya STEM na mgawanyo usio sawa wa kazi za nyumbani kati ya watoto wa kike na wa kiume. Aidha, mdondoko wa watoto wa kike na wavulana umeendelea kuwepo kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ndoa na mimba za utotoni, upungufu wa miundombinu inayozingatia mahitaji ya kijinsia shuleni pamoja na mila na desturi hasi zinazomnyima mtoto wa kike fursa ya elimu. Kwa upande wa wavulana sababu hizo ni pamoja na majukumu ya kutafuta malisho ya mifugo kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, umaskini wa kipato katika kaya na mwamko duni wa kielimu katika ngazi ya kaya.

#### Lengo la Sera

Kukuza usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa elimu bora na mafunzo.

#### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kukuza uelewa wa jamii kuhusu kubadili mitazamo hasi inayowanyima wanawake na wasichana fursa ya kupata elimu katika ngazi zote;

(ii) Kuhamasisha uboreshaji wa miundombinu na vifaa ili iwe rafiki kwa wasichana na wavulana katika Taasisi za Elimu;

(iii) Kuhamasisha ushiriki wa watoto wa kike katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati – (STEM) ikiwa ni pamoja na kuhamasisha kaya na kuendeleza programu za ushauri kwenye Taasisi za Elimu;

(iv) Kuhamasisha ongezeko la udahili na kuwabakiza shuleni wasichana na wavulana na kuendeleza elimu mbadala kwa walioacha shule kwa sababu mbalimbali; na

(v) Kuimarisha hatua za kukabiliana na Ukatili wa Kijinsia, Unyanyasaji wa Kingono kwa wavulana na wasichana, wanawake na wanaume kwenye Taasisi za Elimu.

### 3.2.6 Jinsia na Afya

#### Maelezo:

Afya ya uzazi kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana ni suala muhimu katika jamii. Hata hivyo, upatikanaji wa huduma hizi unakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mila na desturi, hali duni ya kiuchumi, umbali wa vituo vya kutolea huduma, kukosekana kwa huduma bora

za afya na kukosekana kwa lishe bora. Mila na desturi ikiwemo ukeketaji una athari kubwa katika afya ya uzazi hasa pale aliyefanyiwa ukeketaji akifikia wakati wa kujifungua. Kwa Mujibu wa SIGI (2022), unaonesha asilimia 18 ya wanawake waliofanyiwa ukeketaji wamepata changamoto za kiafya ikiwemo changamoto wakati wa kujifungua. Aidha, mila na desturi za Kitanzania zinamnyima mwanamke kuwa na maamuzi juu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango. Kutokana na utafiti huo, asilimia 18 ya wanawake ndio wenye maamuzi binafsi ya kufanya uzazi wa mpango na asilimia 12 ya wanawake ndio walifanya maamuzi ya idadi ya Watoto. Hali hii imekuwa ikiwaathiri zaidi wanawake na wasichana na kusababisha vifo vya mama na mtoto, mimba zisizotarajiwa, kupoteza damu nyingi kipindi cha kujifungua, lishe duni, maambukizi ya magonjwa ya zinaa na mimba za utotoni. Pamoja na jitihada za Serikali kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kujifungulia hospitaliniau katika vituo vya afya, bado kuna changamoto ya wanawake kujifungulia nje ya vituo vya afya. Utafiti huo pia unaonesha kuwa idadi ya wanawake wanaojifungulia nyumbani inaendelea kuwepo hali inayochangia hatari ya vifo vya mama na mtoto kwa kukosa huduma stahiki za kitabibu. Aidha, magonjwa ya saratani ya matiti, shingo ya uzazi na tezi dume yameendelea kuongezeka kutokana na kutokuwa na utamaduni wa kufanya uchunguzi wa afya mara kwa mara. Vilevile, ukosefu wa bima ya afya kwa baadhi ya wananchi wakiwemo wanawake hususan waishio vijijini imekuwa kikwazo kwao kufikia huduma muhimu za afya.

### Lengo la Kisera

Kuhimiza huduma za afya jumuishi zikiwemo afya ya uzazi na magonjwa asiyoambukizwa kwa wanawake na wanaume.

### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kuhimiza uzingatiaji wa mahitaji ya kijinsia katika sekta ya afya na programu zake;

(ii) Kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana katika programu za afya ya uzazi pamoja na afya ya akili;

(iii) Kuhimiza wanawake, wasichana, wanaume na wavulana kuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ili kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa ikiwemo saratani ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume; na

(iv) Kuendeleza na kukuza programu za umuhimu wa lishe bora kwa wanaume na wanawake hususan wanawake wajawazito.

## 3.2.7 Jinsia, Teknolojia na Ubunifu

### Maelezo:

Ubunifu na teknolojia ni nyenzo muhimu katika kuwezesha kufikiwa kwa maendeleo jumuishi na uwezeshaji wanawake. Wanawake na wanaume wanahitaji kuwezeshwa kupata na kutumia teknolojia kwa lengo la kukuza uwezo na maarifa ya kupata masoko, kunufaika zaidi na fursa za kiuchumi, kushiriki katika ufanyaji wa maamuzi, kujenga mtandao wa kibiashara na kupunguza

mzigo wa kazi. Kupitia ubunifu na teknolojia wanawake wameweza kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa zao na kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na ya kimataifa. Wanawake na wasichana ni kundi muhimu linalohitaji hamasa ya kuongeza ubunifu wa kiteknolojia ili kujipunguzia mzigo wa kazi. Hata hivyo, taarifa zinaonesha kuwa udahili wa watoto wa kike katika masomo ya Sayansi na Teknolojia umekuwa mdogo ukilinganisha na watoto wa kiume. Kwa mfano katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela - Arusha ilidahili wanafunzi 539 (wanaume 355 na wanawake 184) mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 722 (wanaume 472 na wanawake 250) waliodahiliwa mwaka 2020. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kilidahili wanafunzi 6,779 (wanaume5,275 na wanawake 1,504) mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 6,137 (wanaume 4,764 na wanawake 1,373) waliodahiliwa mwaka 2020, sawa na ongezeko la asilimia 10.5.

Aidha, wanafunzi 1,176 (wanaume 904 na wanawake 272) walihitimu ikilinganishwa na wanafunzi 1,203 (wanaume 952 na wanawake 251) waliohitimu mwaka 2020. Vilevile, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilidahili wanafunzi 3,581 (wanaume 2,839 na wanawake 742) mwaka 2021 ikilinganishwa na wanafunzi 2,190 (wanaume 1,537 na wanawake 653) waliodahiliwa mwaka 2020.

Pamoja na ushiriki mdogo wa wanawake na wasichana katika taaluma hiyo, imethibitika kuwa kukua kwa huduma za teknolojia ya habari na mawasiliano kumewezesha wanawake kupata kwa urahisi taarifa za masoko, kuwasiliana na kutengeneza mitandao ya kibiashara katika kiwango cha kimataifa. Teknolojia ya habari na mawasiliano pia imechangia katika ukuaji wa elimu, maarifa na maendeleo ya kitaasisi na hivyo kusababisha kuimarika kwa uwezeshaji wa wanawake kijamii, kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi. Aidha, nchini Tanzania matumizi ya teknolojia ya simu za mkononi yameongezeka mijini na vijijini na imekuwa na tija hususan kwa wanawake katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha. Changamoto zinazowakabili wanawake kuhusiana na upatikanaji wa teknolojia ni pamoja na kukosa uelewa wa kina wa matumizi ya teknolojia ya simu za mkononi, upatikanaji duni wa mitandao hususan vijijini, wanawake kushindwa kumudu gharama kubwa za teknolojia ya kilimo mfano trekta, mashine za kupandia na kuvunia pamoja na majiko banifu.

### Lengo la Kisera

Kuimarisha matumizi ya teknolojia katika uwezeshaji wa wanawake na wanaume.

### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kuimarisha mifumo ya kidijitali katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia;

(ii) Kuhamasisha ubunifu na matumizi ya teknolojia za kisasa kwa wanawake na wanaume;

(iii) Kukuza uelewa kwa wanawake juu ya umuhimu wa teknolojia zikiwemo teknolojia zinazopunguza ugumu wa kazi na kuongeza thamani za bidhaa wanazozalisha ili kukidhi viwango vya ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi; na

(iv) Kuimarisha ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuwezesha upatikanaji wa teknolojia rafiki.

### 3.2.8 Takwimu za Kijinsia

**Maelezo:**

Takwimu za kijinsia ni muhimu katika kuwaongoza waandaaji wa mipango na wafanya maamuzi kufahamu hali halisi ya kijinsia na hivyo kuweza kuandaa majibu sahihi ya changamoto zilizopo. Takwimu hizi zinapatikana kutoka katika vyanzo mbalimbali na vilevile zimesambaa na hivyo kuwa vigumu kupatikana kwa taarifa kutoka katika vyanzo vyote. Serikali pamoja na Asasi za Kiraia (AZAKI) na wadau wengine hukusanya takwimu zilizochambuliwa kijinsia, zikihusisha idadi ya watu, masuala ya afya, maendeleo ya jamii, kilimo, uchumi, elimu, huduma za jamii, mazingira, na taarifa kuhusu ajira. Takwimu hizi hukusanywa kupitia sensa ya watu na makazi, tafiti na takwimu za kiutendaji. Nyaraka nyingine nyingi zimebainika kuwa na taarifa muhimu za kijinsia kwa ajili ya uandaaji wa Sera na Programu. Aidha, nyaraka nyingine zimeonekana kutokuwa na taarifa toshelevu za kijinsia na hazijumuishi masuala mapya kuhusu hali ya wanawake na usawa wa kijinsia.

Katika muktadha huu, upo umuhimu wa kujenga uelewa wa masuala ya takwimu kwa sekta zote kuanza kukusanya na kuchakata takwimu kwa kuzingatia masuala ya kijinsia na kutekeleza mpango wa ufuatiliaji na tathmini wenye mtazamo wa kijinsia. Hii itasaidia kuhamasisha ufuatiliaji wa mara kwa mara wa Sera za kisekta, miradi, programu na mipango kwa ufanyaji wa maamuzi yenye tija.

**Lengo la Sera**

Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa takwimu za kijinsia.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha kwamba sekta zote zinakusanya, kutunza, kuchakata, kutumia na kusambaza takwimu zenye mrengo wa kijinsia;

(ii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika kuwezesha upatikanaji wa taarifa zenye kuzingatia uchambuzi wa kijinsia;na

(iii) Kuhamasisha uwekezaji katika tafiti na maendeleo ya jinsia.

### 3.2.9 Wanawake, Amani na Usalama

**kwa Maelezo:**

Kutokana na madhara wanayopata wanawake na wasichana yanayosababishwa na migogoro na majanga ni muhimu kuhamasisha ongezeko la ushiriki wa wanawake katika mifumo ya usimamizi wa usalama katika ngazi zote za jamii ikiwemo mifumo ya usuluhishi na ushiriki katika kulinda amani. Vilevile, ni muhimu kuzingatia masuala ya jinsia katika programu za kuzuia na kudhibiti majanga na migogoro pamoja na kushughulikia ukatili wa kijinsia na kingono wakati wa majanga na migogoro. Aidha, ni muhimu kutambua mchango wa wanawake katika amani na usalama kwa kuhakikisha ushiriki wao kwenye utatuzi wa migogoro pamoja na kujenga jamii upya baada ya migogoro na majanga ya asili yatokanayo na athari za shughuli za binadamu. Mfano, janga la UVIKO 19,

migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji, mafuriko, matetemeko ya ardhi na ukame. Haya yote yanapotokea waathirika wakubwa huwa ni wanawake na watoto ambao ushiriki na nafasi yao katika vyombo vya maamuzi ni mdogo ukilinganishwa na wanaume kwa kuchangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo mila na desturi katika jamii.

**Lengo la Sera**

Kuzingatia masuala ya kijinsia katika mifumo na programu za Wanawake, Amani na Usalama.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kukuza uelewa wa ajenda ya wanawake, amani na usalama kwa jamii;

(ii) Kukuza na kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama kwa kutambua mchango wa wanawake na kuwezesha ushiriki wao katika ngazi zote za maamuzi;

(iii) Kuzuia na kushughulikia ukatili wa kijinsia na kingono wakati wa majanga na migogoro; na

(iv) Kuimarisha programu za ujenzi wa jamii kwa kuzingatia mahitaji ya kijinsia baada ya majanga na migogoro.

### 3.2.10 Masuala Mtambuka

Maendeleo ya jinsia ni suala mtambuka linalotekelezwa kupitia jitihada za sekta mbalimbali. Masuala mtambuka yanayochangia kwa sehemu kubwa katika maendeleo ya wanawake na jinsia ni pamoja na; Jinsia na Mazingira; Jinsia na Utawala Bora; na Jinsia na VVU/UKIMWI.

#### 3.2.10.1 Jinsia na Utawala Bora

**Maelezo:**

Uzingatiwaji wa Misingi ya Utawala Bora ni nyenzo muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia kwa kuhamasisha utawala wa sheria, uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa raia. Ni mbinu muhimu ya kuwezesha kufikiwa kwa uharaka kwa malengo ya maendeleo pamoja na usawa wa kijinsia. Kwa kutambua uhalisia huo, Serikali imetekeleza jitihada mbalimbali zilizolenga kuhamasisha utawala bora na kuongeza ushiriki wa wanawake katika mamlaka za ufanyaji maamuzi kama vile Bunge na Mamlaka za Serikali za Mitaa; uanzishaji wa Dawati la Jinsia katika Vituo vyote vya Polisi na katika Taasisi za Elimu ya Juu; na kuanzisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto nchi nzima. Pamoja na mafanikio haya, masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake hayajapewa kipaumbele katika utekelezaji wa misingi ya utawala bora. Hivyo, sera hii inalenga kuhamasisha uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika misingi ya utawala bora katika sekta zote.

**Lengo la Sera**

Kuhamasisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika misingi ya utawala bora.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kukuza uelewa wa jamii kuhusu utawala bora unaozingatia usawa wa kijinsia; na

(ii) Kuimarisha uwajibikaji, uwazi, ushiriki na utawala wa sheria unaozingatia usawa wa kijinsia.

### 3.2.10.2 Jinsia na VVU/UKIMWI

**Maelezo:**

Maambukizi ya VVU/UKIMWI ni miongoni mwa changamoto zinazosababisha ukosefu wa usawa na haki kwa wanawake. Katika maeneo ambayo kuna maambukizi makubwa ya VVU, ukatiliwa watu walio katika uhusiano, umeonekana kuongeza hatari ya wanawake kupata VVU kwa asilimia 50. Utafiti uliofanywa na NBS, (THIS, 2016/17) kuhusu athari za VVU nchini Tanzania unaonyesha kuwa maambukizi ya VVU kwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 ni mara mbili ya wanaume wenye umri huo. Suala hili husababisha migogoro, ambapo wanawake wanaoishi na VVU wamekuwa mara kwa mara wakiripoti kufanyiwa ukatili kutoka kwa wenza wao, familia na jamii na katika huduma za afya. Utafiti huo unaonesha kuwa kiwango cha maambukizi mapya ya VVU kwa watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi ni asilimia 0.24 (0.16% kwa wanaume na 0.32% kwa wanawake). Kiwango hiki kinakadiriwa kuwa ni idadi ya watu 72,000 kwa mwaka (wanaume 24,000 na wanawake 48,000). Miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 15-49, Maambukizi mapya yanakadiriwa kuwa asilimia 0.24, na wale wenye umri wa miaka 15-64 ni asilimia 0.25 (0.17% ya wanaume na 0.34% ya wanawake). Kwa wanaume, asilimia kubwa ya maambukizi mapya ya VVU ni kwa wale wenye umri wa miaka 35- 49 (0.37%), na kwa wanawake ni kwa wale wenye umri wa miaka 25-34 (0.7%), hii inaonesha ni kwa kiasi gani Serikali inatakiwa kuweka jitihada za makusudiza kutokomeza maambukizi ya VVU nchini.

**Lengo la Kisera**

Kuhimiza uzingatiaji wa huduma kwa Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI pamoja na kujikinga na maambukizi mapya ya VVU kwa wanaume na wanawake.

**Matamko ya Sera**

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo:

(i) Kukuza uelewa juu ya madhara ya VVU/UKIMWI na athari za unyanyapaa kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana; na

(ii) Kuhamasisha uwepo wa mazingira wezeshi na rafiki kwa wanawake na wanaume, wavulana na wasichana kupima, kupata huduma na kubaki kwenye huduma za VVU/UKIMWI.

### 3.2.10.3 Jinsia na Mazingira

**Maelezo:**

Uharibifu wa mazingira kwa kiasi kikubwa huchangiwa na uwepo wa shughuli mbalimbali za kibinadamu mathalani uvunaji wa mazao ya asili, shughuli za viwanda, kilimo, madini, uvuvi na

ufugaji. Shughuli hizi zinapotekelezwa bila kuzingatia kanuni za utunzaji wa mazingira husababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Uhusiano huu wa mazingira na shughuli za kiuchumi huathiriwa na changamoto mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, matumizi mabaya ya rasilimali za asili, uvunaji wa mazao ya asili usiozingatia uhifadhi wa mazingira, matumizi ya mbinu duni za kilimo, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji, kupungua kwa rasilimali za asili kama vile maji na mazao ya misitu yakiwemo kuni na mkaa kwa matumizi ya nyumbani na hivyo kusababisha kuongezeka kwa uzito wa kazi kwa wanawake. Madhara mengine ni pamoja na mahudhurio hafifu/utoro shuleni na kushindwa kuendelea na masomo kwa wanafunzi wa kike na wa kiume kutokana na kujihusisha na utafutaji wa maji, nishati na malisho.

### Lengo la Kisera

Kukuza uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika usimamizi wa mazingira.

#### Matamko ya Sera

Serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya yafuatayo: -

(i) Kuhamasisha usimamizi wa mipango na mikakati ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi kuwa jumuishi ikizingatia masuala ya jinsia; na

(ii) Kukuza uelewa kwa wanawake na wanaume kuhusu umuhimu wa utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuondoa athari hasi kwa wanawake na wasichana.

# SURA YA NNE
# MUUNDO WA KISHERIA

Tanzania ina mfumo wa sheria na udhibiti unaowezesha usimamizi, uratibu na utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023. Utekelezaji wa sera hii utazingatia mifumo mbalimbali inayotambuliwa na sheria ikiwemo; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake, Sheria ya Ndoa, Sura ya 29; Sheria ya Mirathi, Sura ya 352 na tamko la Sheria ya Kimila Na. 4 kupitia Tangazo la serikali Na. 436 la mwaka 1963. Tanzania inathamini haki za binadamu na usawa kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake. Katiba inatoa Msisitizo wa kuheshimu haki za binadamu, usawa na utu na pia inalinda uhuru wa kuishi kwa wanawake na wanaume, kumiliki mali na kujipatia kipato kupitia nguvu zao wenyewe, pamoja na haki ya kufikia matarajio yao kielimu. Utekelezaji wa masuala ya jinsia kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Mwaka 2000 umekuwa ukifanywa kupitia sheria zinazosimamiwa na Wizara za kisekta. Hii ni kutokana na kwamba sera hii haikutungiwa sheria mahsusi ya kusimamia utekelezaji wake.

Upungufu wa mfumo wa kisheria uliobainika unaathiri ufanisi katika kulinda haki na ustawi wa wanawake. Upungufu huo unajumuisha, uwepo wa sheria kinzani hususan katika umiliki wa mali, mirathi na ndoa mfano: Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, Sheria ya Mirathi, Sura ya 352 na Tamko la Sheria za Kimila Na.4 katika T.S. 346/1963. Hata hivyo, matumizi ya Sheria za Kikatiba na za Kimila umewafanya wanawake na wasichana kuwa wahanga wa ubaguzi na ukandamizaji. Pia, Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 zimefanyiwa marekebisho ili kutia hatiani makosa ya ukeketaji na kujamiiana kwa lengo la kuwalinda wasichana walio chini ya miaka 18 dhidi ya ukeketaji na ukatili wa kingono.

Sheria nyingine zinazoathiri upatikanaji wa haki za wanawake nchini kutokana na kuwa na mwelekeo wa kibaguzi inahusisha: Sheria ya Uraia (1995), inayotamka kwamba endapo mwanamke wa kitanzania ataolewa na raia wa kigeni, anapaswa kukana moja kati ya uraia wake kwa sababu Sheria hiyo ya nchi hairuhusu uraia pacha. Kwa hiyo wanawake walioolewa katika utaratibu huu na hawako tayari kukana uraia wao baada ya kuolewa na raia wa kigeni wanaishi katika hali ya utegemezi. Hali hiyo ya utegemezi inawanyima wanawake haki ya kurithi mali za wenza wao. Aidha, Tamko la Sheria ya Kimila Na. 4 ya mwaka 1963 linawapa wanaume haki ya kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika bila masharti. Sheria hii pia inawapa wanawake haki ya kumilikimali zisizohamishika kwa matumizi yao katika kipindi cha uhai wao lakini haiwapi haki ya kuuza malihizo mpaka ambapo hakuna mwanafamilia wa kiume.

Katika kutatua changamoto zilizobainishwa, Serikali kupitia Sera hii itatoa msukumo wa kufanya mapitio au marekebisho ya mfumo wa sheria zenye athari kwa wanawake ikiwemo Sheria ya Ndoa, Sura ya 29, Sheria ya Mirathi, Sura ya 352 na Tamko la Sheria za Kimila Na.4 katika Tangazo la Serikali Na. 346/1963. Katika muktadha huu, Serikali itasimamia utekelezaji wa sheria zote za kikatiba na za kimila ili kuondoa vitendo vya ubaguzi na ukandamizaji dhidi ya wanawake na wasichana.

# SURA YA TANO
# MUUNDO WA KITAASISI

## 5.1 Utangulizi

Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023 inatoa fursa kwa wadau mbalimbali kuwajibika katika utekelezaji wake. Kutokana na masuala ya kijinsia kuwa mtambuka, Sera hii itatekelezwa na Wizara zote za kisekta kwa kuhuisha masuala ya kijinsia katika Sera, Mikakati, Miongozo, Mipango, Programu, na Bajeti zao. Vilevile, ni muhimu kufanya mapitio ya sheria, kanuni na miongozo ya sekta mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa matamko ya Sera hii kwa ufanisi.

Aidha, ushirikiano baina ya wadau wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ni muhimu katika utekelezaji wa Sera hii. Wahusika wakuu wa utekelezaji ni pamoja na Wizara yenye dhamana na masuala ya Kijinsia, Wizara za Kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wadau wengine ni; Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Tafiti na Elimu, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Vyombo vya habari na jamii kwa ujumla. Majukumu na wajibu wa wadau ni kama ifuatavyo:

## 5.2 Majukumu ya Wadau

### 5.2.1 Wizara yenye Dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itaratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023. Majukumu mengine ni pamoja na: -

(i) Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na viwango vya ubora wa huduma zinazotolewa nchini katika ngazi zote;

(ii) Kuhamasisha usawa wa kijinsia na kulinda ustawi na ushiriki wa wanawake katika michakato ya maendeleo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi;

(iii) Kuhamasisha uingizaji wa masuala ya kijinsia katika sekta zote, kuondoa vikwazo vya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni vinavyokwamisha kufikiwa kwa usawa wa kijinsia;

(iv) Kuandaa na kutoa miongozo inayolenga kusimamia programu za ulinzi wa makundi tete ya jamii (social protection) ili kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake;

(v) Kufanya uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu zinazohamasisha kufikiwa kwa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake;

(vi) Kutafuta rasilimali zinazohitajika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sera;

(vii) Kuanzisha mfumo bora na wenye ufanisi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera;

(viii) Kuhakikisha sekta zote zinatekeleza mikakati ya usawa wa jinsia na kutoa taarifa kama ilivyobainishwa katika Mikakati ya Maendeleo ya Taifa, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063 pamoja na Mikatabaya Kikanda na Kimataifa inayojumuisha Mikataba/Itifaki ya EAC, SADC, CEDAW na CSW;

(ix) Kutoa ushauri wa kitaalam na kusaidia utekelezaji ili kufikia usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake;

(x) Kukuza ushirikiano kati ya Serikali, Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi katika utekelezaji wa mikakati ya sera;

(xi) Kuratibu uzalishaji, utunzaji na utoaji wa taarifaya takwimu zilizochambuliwa kijinsia; na

(xii) Kukuza upatikanaji sawa wa huduma ya afya kwa kuandaa mikakati na programu za kushughulikia masuala ya wasichana, wavulana, wanawake na wanaume.

### 5.2.2 Wizara yenye Dhamana na Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuandaa Sera na Miongozo ya Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu yenye mrengo wa kijinsia na maendeleo ya wanawake;

(ii) Kuratibu mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili iweze kuwanufaisha wanawake;

(iii) Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kujiwekea akiba katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (kwa uchangiaji wa hiari); na

(iv) Kufanya utafiti kuhusu hifadhi ya jamii kwa wanawake na wanaume walio kwenye sekta isiyo rasmi.

### 5.2.3 Wizara yenye Dhamana na Fedha

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kutumia takwimu za kijinsia katika uandaaji wa bajeti na uratibu wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kisekta;

(ii) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika;

(iii) Kusimamia Mwongozo wa kuandaa bajeti unaozingatia masuala ya jinsia;

(iv) Kuhakikisha wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wanalengwa katika mipango na maendeleo ya kiuchumi;

(v) Kuhakikisha mipango na bajeti ya Wizara za Kisekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa inaandaliwa kwa kuzingatia mwongozo wa uandaaji wa bajeti wenye mrengo wa kijinsia.

(vi) Kufanya ukaguzi wa masuala ya jinsia katika bajeti na matumizi ya kisekta; na

(vii) Kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2023.

### 5.2.4 Wizara yenye Dhamana na Mazingira

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kutoa elimu juu ya uimarishaji wa usafi wa mazingira kwa wanawake na wanaume;

(ii) Kujumuisha masuala ya kijinsia katika Sera, mipango na programu za uhifadhi wa mazingira; na

(iii) Kukuza uelewa wa jamii kuhusu afya na usafi wa mazingira ili kuzuia na kutokomeza magonjwa.

### 5.2.5 Wizara yenye Dhamana na Maji

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa maji hususan katika maeneo ya vijijini ili kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi; na

(ii) Kupunguza gharama za usambazaji wa huduma ya maji ili kuwezesha wanawake wengi kufikia huduma ya maji

### 5.2.6 Wizara yenye Dhamana na Afya

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo;-

(i) Kuingiza masuala ya Usawa wa kijinsia katika Sera, programu, mipango na bajeti za sekta ya afya;

(ii) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya hususan katika maeneo ya vijijini ili kuboresha afya za wanawake na wanaume na kupunguza vifo vya mama na mtoto;

(iii) Kuhimiza wanawake, wasichana, wanaume na wavulana kuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ili kujikinga na VVU/UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyoambukizwa ikiwemo saratani ya Shingo ya Kizazi, Matiti na Tezi Dume;

(iv) Kukuza Uelewa kuhusu umuhimu wa ushiriki wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana katika programu za afya ya uzazi pamoja na afya ya akili

### 5.2.7 Wizara yenye Dhamana na Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhamasisha kuridhiwa kwa mikataba ya kikanda na kimataifa kuhusu usawa wa kijinsia nauwezeshaji wa wanawake; na

(ii) Kuratibu utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na Kikanda, uandaaji na uwasilishaji wa taarifa na kuratibu ushiriki wa ujumbe wa Serikali katika mikutano ya kikanda na kimataifa.

### 5.2.8 Wizara yenye Dhamana na Ardhi

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kufanya marekebisho ya kisheria ili kuimarisha usimamizi wa haki za wanawake kurithi ardhi;

(ii) Kukuza uelewa na ushiriki wa jamii kuhusu haki za wanawake kurithi ardhi;

(iii) Kuhamasisha marekebisho ya Sheria za Kikatiba na Kimila ili kutatua masuala mbalimbali ya kijinsia hususan haki ya kumiliki ardhi kwa wanawake; na

(iv) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

### 5.2.9 Wizara yenye Dhamana na Kilimo

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuwawezesha wanawake kupata na kutumia teknolojia rahisi na pembejeo bora za kilimo pamoja uzalishaji katika sekta husika;

(ii) Kujumuisha masuala ya jinsia katika sekta ya kilimo ili kuhakikisha wanawake na wanaume wanapata huduma sawa;

(iii) Kuboresha miundombinu vijijini (barabara, zana za umwagiliaji na TEHAMA) ili kukuza sekta ya kilimo na kuimarisha usalama wa chakula na lishe kwa wakulima;

(iv) Kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha (mikopo na ujuzi katika usimamizi wa fedha) kwa wanawake wa vijijini wanaojishughulisha na kilimo na hivyo kuwawezesha kupanua uwekezaji katika sekta hizo ili kukuza kipato chao;

(v) Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ya ndani na nje ya nchi kwa wanawake na wanaume; na

(vi) Kuongeza ushiriki wa wanawake na wanaume katika mnyororo wa thamani ya bidhaa za kilimo ili kuzalisha bidhaa zinazokidhi viwango vya ubora wa masoko ya kimataifa.

### 5.2.10 Wizara yenye Dhamana na Mifugo na Uvuvi

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuwawezesha wanawake kupata na kutumia teknolojia rahisi pamoja na huduma za mifugo na uvuvi ili kuongeza tija ya uzalishaji katika sekta husika;

(ii) Kujumuisha masuala ya jinsia katika sekta ya mifugo na uvuvi ili kuhakikisha wanawake na wanaume wanapata huduma sawa;

(iii) Kuboresha miundombinu vijijini (barabara, maeneo ya malisho) ili kukuza uzalishaji wa sekta ya mifugo na uvuvi;

(iv) Kuongeza upatikanaji wa huduma ya fedha (mikopo na ujuzi katika usimamizi wa fedha) kwa wanawake wa vijijini wanaojihusisha shughuli za ufugaji na uvuvi hivyo kuwawezesha kupanua uwekezaji katika sekta hizo ili kukuza kipato chao; na

(v) Kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mifugo na uvuvi ndani na nje ya nchi kwa wanawake na wanaume.

### 5.2.11 Wizara yenye Dhamana na Michezo

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuingiza masuala ya kijinsia katika sera na programu za sekta ya michezo;

(ii) Kuhakikisha ushiriki sawa na jumuishi kwa wanawake na wanaume katika michezo na kuimarisha miundombinu ya michezo ili kukidhi mahitaji ya jinsi zote; na

(iii) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

### 5.2.12 Wizara yenye Dhamana ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuingiza masuala ya usawa wa kijinsia katika sera, mikakati, mipango, programu na mitaala ya elimu ya ngazi zote;

(ii) Kujenga na kuimairisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule zote na taasisi za elimu ili kuimarisha ushiriki sawa wa wanafunzi (wavulana na wasichana) katika masomo;

(iii) Kuhamasisha ushiriki wa AZAKI, Taasisi za Dini na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sekta binafsi katika kuimarisha miundombinu muhimu ya shule na kutoa msaada wa mahitaji kwa wanafunzi wanaotoka katika familia maskini na wanaoishi katika mazingira magumu;na

(iv) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

### 5.2.13 Wizara yenye Dhamana na Katiba na Sheria

Wizara itakuwa na jukumu la kutunga na kufanya mapitio ya sheria zitakazohakikisha kuwa mahitaji ya kijinsia yanazingatiwa katika maeneo yote ya maendeleo na utoaji wa huduma.

### 5.2.14 Wizara yenye Dhamana na Ulinzi na Usalama

Wizara itakuwa na jukumu la kuzingatia usawa wa kijinsia wakati wa kutoa na kupeleka walinda amani ndani na nje ya nchi na kusimamia masuala ya usalama wa wanawake na wanaume na mali zao katika ngazi zote;

### 5.2.15 Wizara yenye Dhamana na Ujenzi

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

i) Kuratibu na kusimamia upatikanaji wa miundombinu rafiki ya ujenzi yenye kukidhi mahitaji ya Wanawake, wanaume na watu wenye mahitaji maalum; na

ii) Kuratibu ushiriki wa wanawake kwenye kandarasi za ujenzi wa miundombinu.

### 5.2.16 Wizara yenye Dhamana na Uchukuzi

Wizara itakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia upatikanaji wa huduma rafiki za usafirishaji zenye kukidhi mahitaji ya wanawake, wazee, watoto na watu wenye ulemavu

### 5.2.17 Wizara yenye Dhamana na Nishati

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa nishati safi ya kupikia ili kuwapunguzia wanawake mzigo wa kazi;

(ii) Kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya nishati safi na mbadala; na

(iii) Kupunguza gharama za nishati na usambazaji wa huduma ya nishati safi ya kupikia ili kuwezesha wanawake wengi kutumia huduma hiyo.

### 5.2.18 Wizara yenye Dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kusimamia masuala ya usalama wa wanawake na wanaume na mali zao katika ngazi zote;

(ii) Kuimarisha upelelezi wa mashauri yanayohusu vitendo vya ukatili wa kijinsia;

(iii) Kuongeza na kuimarisha madawati ya Jinsia na Watoto kwenye vituo vya Polisi Nchini; na

(iv) Kuimarisha mfumo wa kuwafikisha watuhumiwa wa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika vyombo vya sheria kwa wakati.

### 5.2.19 Wizara yenye Dhamana na Uwekezaji na Mipango

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuandaa mipango ya maendeleo ya Kitaifa yenye kuzingatia masuala ya jinsia na maendeleo ya wanawake; na

(ii) Kuhamasisha wanawake kuwekeza kwenye sekta zenye tija.

### 5.2.20 Wizara yenye Dhamana na Viwanda na Biashara

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kukuza na kutafuta fursa za masoko ndani na nje ya nchi ili kuongeza wigo wa soko la bidhaa za wanawake na wanaume;

(ii) Kujenga uchumi wa viwanda utakaofungua fursa kwa wanawake wajasiriamali kupata bidhaa za bei nafuu na kuuzia malighafi wanazozalisha;

(iii) Kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wanawake na wanaume;

(iv) Kubuni na kusambaza teknolojia rahisi na rafiki kwa wanawake na wanaume ili kuongeza tija katika uzalishaji wa bidhaa;

(v) Kuanzisha maeneo maalum ya viwanda kwa ajili ya wanawake kuzalisha bidhaa mbalimbali; na

(vi) Kuwafungamanisha wajasiriamali na sekta ya viwanda kwa lengo la kuwawezesha kukua zaidi kibiashara na kuwa rasmi.

### 5.2.21 Wizara yenye Dhamana na Utumishi na Utawala Bora

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia usawa katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta zote;na

(ii) Kutoa miongozo inayozingatia usawa wa kijinsia mahali pa kazi.

### 5.2.22 Wizara yenye dhamana na Madini

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Itahakikisha uwepo wa fursa sawa ya ushiriki wa wanawake na wanaume katika sekta ya madini; na

(ii) Kujumiusha masuala ya jinsia katika mipango, programu na mikakati inayoratibiwa na Wizara.

### 5.2.23 Wizara yenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Wizara itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake kuanzia ngazi ya Mikoa hadi Vijiji/Mitaa;

(ii) Kuhakikisha kuwa ngazi zote kuanzia Mikoa hadi Vijiji/Mitaa zinajumuisha masuala ya kijinsia katika mipango na bajeti zake;

(iii) Kuhakikisha kuwa inapokea taarifa za utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake kuanzia ngazi ya Mikoa hadi Vijiji/Mitaa na kuziwasilisha katika Wizara yenye dhamana ya masuala na Jinsia; na

(iv) Kuwezesha upatikanaji wa rasilimali za kutekeleza programu na mipango ya inayozingatia masuala ya kijinsia.

### 5.2.24 Sekretarieti za Mikoa

(i) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera hii katika Halmashauri za Mkoa husika;

(ii) Kuhakikisha Halmashauri katika Mkoa zinajumuisha masuala ya kijinsia katika mipango yake;

(iii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera;

(iv) Kuhakikisha upatikanaji wa kanzidata zenye mtazamo wa kijinsia katika ngazi za Halmashauri zilizo chini ya Mikoa husika; na

(v) Kuratibu programu za kuelimisha jamii kupinga aina zote za ukatili katika Halmashauri za Mkoa husika.

### 5.2.25 Mamlaka za Serikali za Mitaa

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa bima za afya kwa wanawake na wanaume wasiokuwa na uwezo;

(ii) Kuweka mipango ya huduma za kijinsia katika Halmashauri;

(iii) Kuanzisha programu za kuelimisha wananchi kujiwekea akiba katika mifumo rasmi ya hifadhi ya jamii;

(iv) Kuratibu na kuimarisha ushirikiano na wadau wanaotoa huduma za kijinsia;

(v) Kuwashirikisha wanawake katika mipango ya maendeleo ya Halmashauri;

(vi) Kutunga Sheria ndogo kwa ajili ya kulinda haki, ustawi na maendeleo ya jinsia;

(vii) Kuandaa programu za kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kupinga aina zote za ukatili;

(viii) Kuandaa programu za kuelimisha jamii kuhusu mila na desturi zinazokiuka haki na ustawi wa wanawake; na

(ix) Kuandaa, kutunza na kuhuisha takwimu kijinsia.

### 5.2.26 Bunge

(i) Kutunga sheria za kuhamasisha usawa wa kijinsia na kuzuia ubaguzi;

(ii) Kufanya marekebisho au kufuta sheria kandamizi kwa wanawake na wasichana;

(iii) Kuimarisha uzingatiaji wa kanuni ya kikatiba ya asilimia 30 ya uwakilishi katika nafasi za uongozi;

(iv) Kuhakikisha michakato ya kibajeti ya Kitaifa, Kisekta na Halmashauri inazingatia masuala ya kijinsia;

(v) Kutoa taarifa kuhusu uzingatiaji wa masuala ya usawa wa kijinsia na utekelezaji wa kanuni za kuzuia ubaguzi;

(vi) Kuhakikisha ushiriki sawa wa kijinsia katika kuibua, kuidhinisha na kutekeleza miradi ya maendeleo; na

(vii) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

### 5.2.27 Asasi za Kiraia/Bodi za Kitaalam

AZAKI na Bodi za Kitaalam zitakuwa na jukumu kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

(i) Kuingiza masuala ya kijinsia katika mipango, programu na mikakati ya taasisi husika;

(ii) Kukuza na kutetea haki za wanawake, wanaume, wasichana na wavulana kwa kuzingatia misingi ya mila na desturi za Taifa letu;

(iii) Kuhamasisha ushiriki sawa wa wanawake na wanaume katika ngazi mbalimbali za maamuzi ikiwa ni pamoja na Vyama vya Siasa;

(iv) Kuhamasisha utengaji wa bajeti kwa ajili ya mahitaji ya makundi maalum katika jamii hususan watu wenye ulemavu, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na watu wanaoishi na VVU/UKIMWI;

(v) Kuandaa na kutekeleza programu za kuhamasisha usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake;

(vi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa afua za masuala ya kijinsia;

(vii) Kuhakikisha bajeti za taasisi husika zinazingatia masuala ya kijinsia; na

(viii) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

#### 5.2.28 Sekta Binafsi

Sekta binafsi zitakuwa na jukumu kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

(i) Kuchukua hatua madhubuti za kukuza usawa wa kijinsia katika majukumu ya kitaasisi;

(ii) Kuhamasisha wanawake na wasichana kujifunza Taaluma ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati - STEM ili kunufaika na fursa za ajira zinazotokana na taaluma husika;

(iii) Kusaidia ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu za kijinsia;

(iv) Kuandaa na kutekeleza Sera za usawa wa kijinsia mahali pa kazi ili kuwalinda wafanyakazi hasa wanawake dhidi ya aina mbalimbali za unyanyasaji;

(v) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya usawa wa Kijinsia katika Taasisi husika;

(vi) Kuingiza masuala ya Jinsia katika Sera na mipango ya Taasisi husika;

(vii) Kutoa motisha na kuwasaidia wanawake wajasiriamali;

(viii) Kushughulikia tofauti za kijinsia kupitia ajira, upatikanaji wa rasirimali na kufanya maamuzi;

(ix) Kuandaa na kutekeleza programu ya kurejesha sehemu ya mapato kwa jamii- CSR ili kuchangia kwenye malengo ya Sera hii;

(x) Kuchangia bajeti ya utekelezaji wa Sera hii; na

(xi) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

#### 5.2.29 Taasisi za Elimu na Utafiti

Taasisi za Elimu na Utafiti zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kufanya tafiti kuhusu masuala ya usawa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

(ii) Kuanzisha na kutekeleza programu za ushirikishaji jamii na uanagenzi zinazozingatia usawa wa kijinsia;

(iii) Kutafuta na kutenga rasilimali zinazohitajika kufanya tafiti na kutoa taarifa ya matokeo ya tafiti ili kuwezesha utekelezaji wa Sera hii;

(iv) Kuandaa mafunzo na programu za elimu kwa jamii kuhusu usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

(v) Kutokomeza ukatili wa kijinsia kupitia mipango, programu na mikakati mbalimbali;

(vi) Kutoa huduma za ushauri elekezi katika masuala ya usawa wa kijinsia; na

(vii) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za

uongozi na maamuzi katika sekta husika.

### 5.2.30 Wadau wa Maendeleo

Wadau wa maendeleo watakuwa na jukumu kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kutekeleza majukumu yafuatayo: -

(i) Kuimarisha ushirikiano na Serikalina kuratibu wadau wa maendeleo wanaojihusisha na masuala ya Jinsia;

(ii) Kutenga rasilimali ili kuwezesha utekelezaji wa sera hii;

(iii) Kushirikiana na Serikali katika kuimarisha mifumo ya uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya Sera hii;

(iv) Kuwezesha kufanyika kwa tafiti mbalimbali zinazolenga kubainisha hali ya usawa wa kijinsia nchini;

(v) Kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazolenga kukuza usawa wa kijinsia; na

(vi) Kuwezesha upatikanaji wa maarifa, kubadilishana ujuzi na uwekezaji katika tafiti za kijinsia

### 5.2.31 Vyombo vya Habari

Vyombo vya habari ni wadau muhimu katika juhudi za kukuza usawa wa kijinsia. Vitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuhamasisha usawa wa kijinsia katika ngazi zote za jamii;

(ii) Kuhamasisha misingi ya utawala bora inayozingatia usawa wa kijinsia;

(iii) Kuibua na kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia;

(iv) Kuelimisha jamii kuhusu ya mikakati mbalimbali ya kukuza usawa wa kijinsia;

(v) Kutangaza na kutoa machapisho mbalimbali kuhusu tafiti na matokeo ya tafiti zenye mrengo wa kijinsia; na

(vi) Kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika ajira na kufikia katika nafasi za uongozi na maamuzi katika sekta husika.

### 5.2.32 Familia na Jamii

Familia na Jamii ni wadau wakuu katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake yaMwaka 2023, kutokana na ushiriki wao katika malezi na makuzi ya watoto. Wanawake na Wanaume ndiyo wanufaika wakuu wa Sera hii katika ngazi ya jamii kwakuwa maamuzi mengi hufanyika katika ngazi ya kaya/familia. Hivyo, ushiriki wa wanawake, wanaume na makundi maalumu kama vile wasichana, wazee, na watu wenye ulemavu katika utekelezaji wa Sera hii ni muhimu ili kuwezesha utatuzi wa changamoto katika ngazi ya jamii.

## 5.3 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ni kipengele muhimu katika utekelezaji wa Sera hii. Kwa kuzingatia kwamba masuala ya kijinsia ni mtambuka na utekelezaji wake unahusisha sekta mbalimbali, hivyo ufuatiliaji

na tathmini utafanyika kupitia Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali zinazotekeleza sera hii. Aidha, Wizara yenye dhamana na masuala ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum itakuwa na jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa sera hii katika ngazi ya Taifa.

Ufuatiliaji na tathmini utahusisha: kufanya tafiti za awali (baseline surveys), kufuatilia mwenendo wa ufikiwaji wa malengo kwa kila eneo la Sera, na kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kama ulivyobainishwa katika Mkakati wa Utekelezaji wa Sera. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo na shabaha utafanyika katika vipindi mbalimbali ikihusisha mapitio ya mwaka yatakayojikita katika kutathmini kama afua zilizopangwa zinaendana na mafanikio yaliyopatikana katika kila shabaha. Vilevile, tathmini itahusisha mapitio ya taarifa za tafiti mbalimbali na maoni ya wanufaika wa Sera kulingana na matokeo yaliyofikiwa katika kipindi cha mapitio.

Vipengele vya ufuatiliaji na tathmini vitalenga: -

(i) Kusaidia wadau kutekeleza Sera kwa kuzingatia mipango, programu na mikakati ya Sekta/ Mashirika mbalimbali na kuandaa viashiria vya matokeo vyenye mtazamo wa kijinsia kwa mtu binafsi, familia na jamii;

(ii) Kuimarisha ushirikiano na AZAKI ili kubaini maeneo ya vipaumbele vya kila shirika na hivyo kuondoa mwingiliano wa majukumu;

(iii) Kuandaa viashiria vya kijamii vya kupima usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake;

(iv) Kuandaa viashiria vinavyozingatia usawa wa kijinsia na umaskini katika ngazi ya mtu binafsi, familia, utawala na kwa jamii kwa ujumla;

(v) Kuwezesha kufanyika kwa uratibu na tathmini ya kina ya mfumo wa matokeo ya jitihada na afua za uingizaji wa masuala ya kijinsia kuendana na mikakakti ya Sera;

(vi) Kuongeza ushiriki wa jamii katika muundo wa uongozi wa programu za ulinzi na ustawi wa jamii ili kuipajamii uwezo wa kuwajibisha mamlaka husika;

(vii) Kutathmini miradi yote ya ulinzi na ustawi wa jamii na programu ili kubaini kama zinaendana na shabaha za sera na matarajio ya kufikia usawa wa kijinsia na uwezesha wanawake;

(viii) Kuweka kumbukumbu za taarifa na takwimu mbalimbali kuhusu masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake; na

(ix) Kutathmini utoshelevu wa rasilimali na mgao wa kibajeti katika shabaha zilipangwa.

Mkakati wa ufuatiliaji na tathmini utahusisha: -

(i) Kukusanya taarifa za kila mwezi kutoka kwa taasisi zote zinazotekeleza mikakati ya sera hii;

(ii) Kufanya ufuatiliaji wa kila mwaka na ukaguzi wa ubora wa huduma zinazotolewa katika jamii; na

(iii) Kufanya mapitio ya kila mwaka ya utekelezaji wa sera pamoja na tathmini ya uwezo wa kitaasisi.

## 5.4 Hitimisho

Sera hii ni matokeo ya mapitio ya Sera ya Mwaka 2000 na Mikataba/Itifaki za kikanda na kimataifa ambazo Tanzania imeridhia. Katika kutekeleza malengo ya mikataba na itifaki hizo, Serikali imeweka mikakati ya uingizaji wa masuala ya kijinsia yenye lengo la kuhamasisha usawa wa kijinsia kote nchini. Katika muktadha huu, Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum ilipewa jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera hii na mkakati wake wa mwaka 2005. Hivyo, jitihada za kuimarisha uingizaji wa masuala ya kijinsia katika Sera na mikakati ya Wizara za Kisekta ni muhimu katika kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya usawa wa kijinsia.

Lengo kuu la Sera ni kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza ubaguzi katika ngazi zote za jamii. Sera hii inalenga zaidi kuhamasisha, kutoa miongozo na maelekezo kwa wadau wote katika kupanga, kuandaa Sera, kutenga rasilimali, kutekeleza na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya programu zenye mtazamo wa kijinsia. Vilevile, inatoa msukumo katika jitihada za kupunguza umaskini wa kaya ili kuimarisha hali ya maisha ya jamii.

Aidha, Sera inalenga kuimarisha uwezo wa Wizara yenye dhamana ya masuala ya jinsia kuwa na ufanisi katika uratibu na utekelezaji wa Sera. Kuendelea kukosekana kwa usawa wa kijinsia na kukosekana kwa uwakilishi sawa wa wanawake katika nafasi za kufanya maamuzi katika ngazi zote ni miongoni mwa masuala yanayohalalisha uhitaji wa Sera hii ili kuweka mfumo wa kushughulikia upungufu wa kisera uliobainika. Utekelezaji wa Sera hii utahitaji dhamira na uwajibikaji wa dhati wa Serikali na wadau wote.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, jinsia, wanawake na Makundi Maalum**

Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya, S.L.P 573, 40478 Dodoma, Tanzania.
Telephone: Kituo cha Huduma kwa Wateja (+255 734 986 503, +255 26 2160250)
Nukushi: Fax +255 26 2963348
Barua pepe: ps@jamii.go.tz